Jumamosi Juni 5, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0580602

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Benteke ajifunga Crystal Palace hadi 2023**

UKURASA 20

**Madereva** 50 wafutiwa leseni, warudi darasani

UKURASA 4



**Serikali** yaja na mikakati 8 tatizo la ajira

UKURASA 8

# SABAYA KORTINI

• **Akosa** dhamana baada ya kusomewa mashtaka ya uhujumu uchumi, utakatishaji, unyang'anyi wa kutumia silaha... *Endelea ukurasa 2*



Mkuu wa Wilaya ya Hai aliyesimamishwa kazi, Lengai Ole Sabaya (kulia) na walinzi wake, wakiwa chini ya ulinzi wa maofisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, jana kabla ya kusomewa mashtaka sita ya uhujumu uchumi na unyang'anyi wa kutumia silaha. **PICHA: ALLAN ISACK**

## YALIYOMO

UKURASA WA 5

### SERIKALI YAPIGA 'STOP' KUSAFIRISHA NGURUWE

NGURUWE 12 wamethibitika kufa kutokana na homa ya nguruwe Manispaa ya Morogoro na serikali...

UKURASA WA 17

### MBARONI WAKIDAIWA KUWAVAMIA MASISTA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu tisa kati ya 12 wanaotuhumiwa kuvunja...

UKURASA WA 17

### TEMBO, SIMBA WAFUNGWA MIKANDA YA MAWASILIANO

WIZARA ya Maliasili na Utalii katika kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali...



Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), akifafanua jambo kwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (katikati), alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, Mikocheni Viwandani, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga (wa pili kushoto), Meneja Rasilimali Watu Mwandamizi, Ayoub Semvua (wa pili kulia) na kulia ni Meneja wa Sheria na Rasilimali Watu, Emmanuel Matondo. **Picha zaidi Uk. 7. PICHA: MIRAJI MSALA**

## Mulamula apongeza vyombo vya IPP

UKURASA 2

## Watalii wanavyomimika Tanzania licha ya corona

UKURASA 3



**MICHEZO** SIMBA YAHITAJI POINTI 10 BARA UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Samia amuaga Balozi wa China

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan, jana ameagana na aliyekuwa Balozi wa China nchini, Wang Ke ambaye amemaliza kipindi chake.

Katika mazungumzo yaliyofanyika Ikulu Chamwino mkoani Dodoma, Rais Samia amemshukuru Balozi Wang Ke kwa jitihada zake za kuendeleza na kukuza uhusiano wa Tanzania na China ambao umewezesha kutekelezwa kwa miradi mbalimbali iliyofadhiliwa na China nchini ikiwamo maktaba ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, jengo la Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, jijini Dar es Salaam na msaada wa Sh. bilioni 35 zilizoelekezwa katika miradi ya maendeleo.

Rais Samia pia amemshukuru kwa ufadhili wa China katika miradi mbalimbali ya ujenzi wa miundombinu na uboreshaji wa huduma za kijamii pamoja na ushirikiano wa kibiashara na uwekezaji ambao pamoja na kukuza pato la nchi umesaidia Watanzania wengi kupata ajira.

Rais Samia pia, amepokea salamu za Rais wa China Xi Jinping na kumtakia yeye na Wachina wote maadhimisho mema ya miaka 100 ya Chama cha Kikomunisti cha China (CPC), Julai 1, 2021 na shukrani kwa uhusiano na ushirikiano mzuri kati ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na CPC, na Tanzania na China uliodumu kwa miaka 56.

Alisema anatambua kazi kubwa iliyofanywa na CPC katika kuijenga China, na kuimarisha uhusiano wake na mataifa mbalimbali ikiwamo Tanzania na amemhakikishia kuwa nchi yake itaendeleza na kukuza zaidi uhusiano na ushirikiano huo. Kwa upande wake Wang Ke, amemshukuru Rais Samia kwa ushirikiano mkubwa alioupata kutoka serikalini wakati wote wa kipindi chake na kupokea kijiti cha urais kutoka kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dk. John Magufuli.

Katika salamu za Rais wa China Xi Jinping, amesema ana imani kubwa kuwa Rais Samia atafanya mazuri na makubwa kwa Tanzania kutokana na dhamira yake ya kuendeleza kazi nzuri iliyofanywa na Hayati Dk. Magufuli hususani uendelezaji wa miradi ya kimkakati, kuchukua hatua madhubuti za kuboresha mazingira ya kufanya biashara na kuchukua hatua za kisayansi za kukabiliana na janga la ugonjwa wa corona (Covid-19).

Amesema China itaunga mkono juhudi zinazofanywa na Rais Samia na katika kukabiliana na ugonjwa wa corona.



Rais Samia Suluhu Hassan, akiwa katika mazungumzo na Balozi wa China Tanzania, Wang Ke, aliyefika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma jana, kwa ajili ya kuaga baada ya kumaliza muda wake wa kazi hapa nchini. **PICHA: IKULU**

# Sabaya kortini, akosa dhamana

Na Allan Issack, ARUSHA

ALIYEKUWA Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, amepandishwa kizimbani akikabiliwa na makosa matano ya uhujumu uchumi, rushwa, kuongoza genge la uhalifu, utakatishaji wa fedha na unyang'anyi wa kutumia silaha.

Ole Sabaya, msaidizi wake na walinzi wake, walifikishwa kwa nyakati tofauti jana mbele ya mahakimu wa mahakama mbili tofauti za Arusha, kujibu mashtaka yanayowakabili.

Jana mchana, Ole Sabaya na washtakiwa wengine wanne akiwamo msaidizi wake, Silvester Stanslaus, Enock Togolani, John Odemba, Daniel Gabriel na Waston Mwakomange, walifikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha na kusomewa mashtaka yanayowakabili.

Ole Sabaya na wenzake, walisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Martha Mahumbuga.

Akisoma hati ya mashtaka, Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, alidai Ole Sabaya na wenzake wanakabiliwa na shitaka la kwanza la kuongoza genge la uhalifu.

Ole Sabaya, Enock Togolani, Waston Mwakomange, Silvester Stansilaus na John Odemba kwa pamoja, Januari 20 mwaka huu katika maeneo mbalimbali Wilaya ya Arusha, akiwa ofisa wa umma mwenye mamlaka ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, anadaiwa kukiuka majukumu yake ya kiofisi na kwa kutumia mamlaka yake, walijipatia manufaa ambayo kinyume cha sheria.

Katika shitaka la pili linamkabili mshtakiwa wa kwanza, Ole Sabaya, anadaiwa kushiriki vitendo vya rushwa kinyume.

Wakili Chavula alidai washtakiwa Ole Sabaya na Stansilaus, Februari 9 mwaka huu, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba fedha Sh. 390,000 mali ya Bakari Msangi na baada ya wizi huo walimfunga pingu, wakampiga makofi, mateke, ngumi na wakatumia bunduki, kumtisha ili wabaki na fedha walizochukua kutoka kwake.

Ilidaiwa mahakamani huko kuwa Ole Sabaya na wenzake; Silvester na Daniel, Februari 9 Mwaka huu, wakiwa Mtaa wa Bondeni jijini Arusha, waliiba simu moja aina TEKNO na fedha Sh. 35,000, mali ya Ramadhan Rashid.

Katika shtaka lingine linalomkabili Ole Sabaya linalohusu vitendo vya rushwa, inadaiwa Januari 20, mwaka huu, akiwa katika eneo la kwa Morombo, Wilaya ya Arusha, alijipatia fedha kwa mtu aliyetambulika kwa majina ya Francis Mroso, kwa nia ya kumsaidia kukwepa matendo ya kijinai ya ukwepaji wa kodi.

Shtaka la nne la utakatishaji fedha, linawakabili washtakiwa wote, wakidaiwa kutenda kosa Januari 20 mwaka huu maeneo ya kwa Murombo jijini Arusha kwa kujipatia Sh. milioni 90 kwa njia ya uhalifu.

Baada ya washtakiwa wote kusomewa makosa hayo, Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Martha Mahumbuga, alisema mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo na kuahirisha kesi hiyo hadi Julai 18 mwaka huu itakapotajwa tena.

Washtakiwa hao walikana mashtkana hayo na walipelekwa katika mahabusu ya Gereza la Kisongo.

Katika hatua nyingine, mahakama hiyo pia iliarifiwa kuwa washtakiwa hao wanakabiliwa na makosa mengine ya jinai katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Arusha.

Akisoma mashtaka hayo, mbele ya Hakimu wa Mkazi wa Mahakama hiyo, Salome Mshasha, Wakili wa Serikali, Tarsila Gervas, alidai kuwa washtakiwa hao kwa pamoja walitenda makosa matatu ya jinai yakiwamo ya unyang'anyi wa kutumia silaha,

Wakili wa Serikali alipomaliza kusoma maelezo ya kosa, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Salome Mshasha, alisema kwa kuwa makosa hayo hayana dhamana, washtakiwa watakaa mahabusu ya Gereza Kuu la Kisongo hadi Julai 18, mwaka huu itakapotajwa tena.

# Mulamula apongeza vyombo vya IPP

Sabato Kasika na Enock Charles

VYOMBO vya habari vinavyomilikiwa na kampuni ya IPP, vimepongezwa kwa kuzingatia maudhui na weledi katika kuelimisha jamii kupitia vyombo hivyo.

Waziri wa Mambo ya Nje ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula, alitoa pongezi hizo alipotembelea vyombo hivyo, Mikocheni jijini Dar es Salaam, jana. Alisema amefurahishwa na utendaji wa vyombo hivyo na kuahidi kuwa wizara yake itaendelea kutoa ushirikiano kwa kuwa serikali ni rafiki wa vyombo vyote vya habari.

Alisema, yeye ni mdau msomaji wa magazeti ya Nipashe Gaurdian na pia ni msikilizaji mzuri wa vipindi mbalimbali vya Radio One, ITV, East Africa Radio na EATV.

"Wizara yangu itaendelea kushirikiana kwa karibu na vyombo vya habari kwa kuwa vina umuhimu kwa maendeleo ya nchi na hata kuitambulisha vyema Tanzania kwa mataifa mengine," alisema.

Alisema, vyombo vya habari vimekuwa vikifanya kazi kubwa ya kuwahabarisha wananchi kuhusu mambo mbalimbali yakiwamo ya kijamii, kiuchumi kibiashara na kisiasa, hivyo serikali inaunga mkono juhudi hizo.

"Nimefurahishwa kwa jinsi ambavyo mnazingatia weledi wa taaluma na hivyo kuwawezesha wananchi kujua mambo mbalimbali yanayoendelea katika nchi yao, serikali inaheshimu na kuthamini mchango wenu," alisema. Balozi Mulamula alisema, vyombo vya habari pia ni kiungo muhimu ambacho kinaweza kutoa mambo mazuri ya Tanzania na kuyafikisha nje na kutoa mengine ya nje na kuyafikisha kwa Watanzania.

Akizungumzia Watanzania wanaoishi nje ya nchi (Diaspora), alisema serikali inathamini mchango wao na kwamba itajitahidi kwa kadri inavyowezekana kuwaondolea vikwazo ikiwamo kuandaa sera ya mambo ya nje ili kutumia mawazo yao yaweze kuleta faida katika taifa.

Balozi Mulamula alitaka wananchi kuwathamini Watanzania wenzao waliopo nje ya nchi badala ya kuwabagua jambo linaloweza kusababisha kuukosa mchango wao kwa taifa. Pia, alisema wapo waliosoma nje na kupata ujuzi mkubwa ambao unaweza kuwa na manufaa makubwa kwa taifa na kubainisha kuwa hata serikali kuna wakati huwatafuta baadhi yao warejee nchini kutoa mchango kulingana na taaluma zao.

"Kwa mfano Mkurugenzi Mkuu wa TPDC, huyu alikuwa ni mwana Diaspora, wakati ule nikiwa balozi Washington, Marekani tuliwafuata, tukasema tunaanzisha hii sekta kubwa ya mafuta na gesi sasa nyinyi mpo Texas, kwanini msije mkasaidia nchi yetu."

HABARI KITAIFA

## LICHA YA CORONA:

# Watalii wamiminika nchini Tanzania

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Maliasili na Utalii imebainisha kuwa licha ya janga la corona, imevuka lengo lake la kupokea watalii kutoka makisio ya watalii wa nje 437,000 hadi 620,867.

Waziri wake, Dk. Damas Ndumbaro, alibainisha hayo jana bungeni jijini Dodoma alipowasilisha makadirio na mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22. Alisema watalii wa ndani waliowapokea ni 571,353 ambao waliotembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Dk. Ndumbaro alisema kuwa mwaka jana wizara ilitarajia kupokea jumla ya watalii 1,867,000 yakiwa ni makisio kabla ya kutokea kwa janga la corona.

"Baada ya mlipuko wa corona, wizara ilifanya tathmini ya athari za ugonjwa huu katika Sekta ya Utalii na kuweka makisio mapya ya jumla ya watalii 437,000 yaliyozingatia hali halisi ya uwapo wa ugonjwa huo," alisema.

Waziri huyo alisema kutokana na mikakati waliyoiweka baada ya kutokea kwa janga hilo, kwa mwaka 2020, nchi ilifanikiwa kupata watalii 620,867 wa kimataifa na watalii 571,353 wa ndani.

Alisema Tanzania imefanikiwa kuwa miongoni mwa nchi chache za Afrika zilizopata muhuri wa Safe Travel wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (WTTC) kwa kigezo cha hatua za kukabiliana na maambukizi ya corona. Muhuri huo hutolewa kwa kuzingatia nchi husika kutoa mwongozo wa kiafya wa kuzingatiwa na wasafiri wanaoingia na kutoka nchini. Alitaja kigezo kingine ni utayari wa kupokea wageni ili kuwajengea imani watalii katika masoko ya kimataifa kuwa Tanzania ni mahali salama kutembelea.

Pia alisema nchi imeendelea kufungua masoko mapya ya utalii ikiwamo Urusi, Poland na Ukraine na kuorodheshwa na nchi ya Urusi kuwa miongoni mwa nchi tatu duniani ambazo ni salama kwa wananchi wake kutembelea.

Hata hivyo, Waziri Ndumbaro alibainisha kuwa janga la corona limeathiri ukusanyaji wa maduhuli ya wizara ambapo katika mwaka wa fedha 2020/21, ilikadiria kukusanya Sh. bilioni 218.5 kutoka vyanzo inavyovisimamia lakini hadi Aprili mwaka huu, makusanyo ni Sh. bilioni 147.2, sawa na asilimia 67 ya lengo.

Alisema taasisi za wizara ambazo makusanyo yake yanapitia Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa maana ya Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCAA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) ziliidhinishiwa kukusanya Sh. bilioni 584.6. "Hadi mwishoni mwa Aprili mwaka huu, taasisi hizi zilikusanya jumla ya Sh. bilioni 89.5, sawa na asilimia 15 ya lengo la makusanyo.

"Kutofikiwa kwa malengo hayo kulisababishwa kwa kiasi kikubwa na uwapo wa mlipuko wa ugonjwa wa corona," Dk. Ndumbaro alifafanua.

Waziri huyo aliliomba Bunge kuidhinisha Sh. bilioni 571.6 kwa ajili ya makadirio ya matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

●**Soma hotuba ya Waziri Ndumbaro Uk. 11-15.**

# Ujangili wafyekwa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI imepunguza matukio ya ujangili kwa takriban asilimia 90 na kuzuia matukio 302 kabla hayajatendeka.

Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo jana bungeni jijini Dodoma alipowasilisha makadirio na mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Alisema wizara imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa shughuli za kilimo, ufugaji na makazi.

Alisema matokeo ya sensa ya mwaka jana yameonyesha kuongezeka kwa idadi ya tembo katika Mfumo Ikolojia Serengeti kutoka 6,087 mwaka 2014 hadi 7,061 mwaka 2020.

"Mafanikio ya kupungua kwa ujangili, uvunaji haramu wa mazao ya misitu na kuongezeka kwa wanyamapori yamechangiwa pamoja na mambo mengine, kuendeshwa kwa doria 746,413 zilizowezesha kukamatwa kwa watuhumiwa 5,609; kuvunjwa kwa mitandao 95 ya ujangili; na kuzuiliwa kwa matukio 302 ya ujangili kabla hayajatendeka," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema jitihada nyingine ni pamoja na ujenzi wa minara mitatu ya mawasiliano ya redio katika maeneo ya Oldeani, Losirwa na Kreta ya Empakai.

"Kutokana na juhudi hizi, ujangili umepungua kwa takriban asilimia 90," waziri huyo alibainisha.

**MIMEA VAMIZI**

Kuhusu mkakati wa kitaifa wa kudhibiti mimea vamizi katika hifadhi 2019/29, Dk. Ndumbaro alisema wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kufanya utafiti kuhusu mtawanyiko, madhara na kubaini mbinu za kukabiliana na mimea hiyo.

Alisema katika hatua za awali, imebainika uwapo wa aina 25 za mimea vamizi ndani ya eneo la Hifadhi ya Ngorongoro.

Waziri Ndumbaro alisema utafiti uliofanywa na Chuo Kikuu cha Nelson Mandela umebaini njia ya asili ya kudhibiti mimea vamizi aina ya Gutenbergia cordifolia, Tagetes minutana Bidens schimperi, inayopatikana katika Kreta ya Ngorongoro na eneo la Ndutu.

Alisema pamoja na mbinu hizo, wizara imeendelea kutumia mbinu nyingine za kupambana zikiwamo kung'oa na kufyeka mimea hiyo.

"Hatua hizi zimewezesha kutokomeza gugu karoti kwa zaidi ya asilimia 90, kudhibiti mimea mingine vamizi kwa asilimia 15.6 kwenye eneo la Kreta ya Ngorongoro lenye ukubwa wa hekta 5,301 ambalo imeathirika na mimea hii," alisema.

Waziri huyo alisema wamefanikiwa kuondoa mimea vamizi kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 2,269 katika hifadhi za Taifa za Arusha, Kitulo, Serengeti, Katavi, Milima ya Mahale, Ziwa Manyara, Mikumi, Milima ya Udzungwa, Ibanda -Kyerwa, Rumanyika -Karagwe, Tarangire, Gombe, Kitulo, Kisiwa cha Saanane na Kilimanjaro kwa lengo la kuboresha maeneo ya malisho.

"Jumla ya miti ya asili 2,700 imeoteshwa katika hifadhi za Taifa Kilimanjaro na Kitulo katika maeneo ambayo mimea vamizi imeng'olewa," alisema.

Mwishoni mwa mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti mbili kuhusu Sekta ya Utalii na Uhifadhi; moja ikiangazia ujangili ulivyodhibitiwa nchini na nyingine ikigusia mimea vamizi na utupaji taka ndani ya hifadhi za taifa.



# Marekani ya ufadhili mil. 16/- ujenzi vyoo

**Na Mwandishi Wetu**

UBALOZI wa Marekani, kupitia Mfuko wa Balozi wa Kusaidia Miradi ya Kijamii, umefadhili ujenzi wa vyoo vilivyo rafiki wa mazingira vilivyojengwa kwa matofali maalumu rafiki wa mazingira katika Shule ya Msingi Karume wilayani Temeke.

Uzinduzi rasmi wa vyoo hivyo uliofanywa jana na Balozi Donald Wright na Ofisa Elimu wa Wilaya ya Temeke Rashid Ally, katika maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani, ambayo huadhimishwa kimataifa Juni 5.

Vyoo hivyo vimejengwa kwa kutumia ruzuku ya Dola za Kimarekani 7,000 (Sh. mil. 16.2) kutoka katika Mfuko wa Balozi wa Kusaidia Miradi ya Kijamii, mfuko unaoendeshwa na Ubalozi wa Marekani kusaidia miradi midogo inayolenga kuisaidia na kuihimiza jamii kujitegemea.

Ruzuku hiyo ilitolewa kwa asasi isiyo ya kiserikali ya PHEDES, inayoongozwa na Mkurugenzi John Ambrose na Meneja mradi Hellen Sailas.

Helen ni mjasiriamali wa mazingira ambaye amebuni mbinu ya kutengeneza matofali kwa kuyeyusha taka za plastiki zilizookotwa katika fukwe za Dar es Salaam. Kutokana na ruzuku hiyo, hivi sasa Hellen ameweza kuanzisha kampuni ya Arena Recycling Industry ili kuzalisha matofali zaidi.

Akizungumza katika hafla hiyo, Balozi Wright alisema, jitihada za kulinda mazingira zinaweza pia kuzalisha fursa mpya.

"Ninaipongeza jamii na PHEDES kwa ubunifu na wazo la kutatua matatizo mawili kwa wakati mmoja – yaani tatizo la uchafuzi wa bahari kutokana na takataka za plastiki na lile la kukosekana mfumo wa maji na usafi. Nimefurahishwa pia na maono ya Hellen ya kusafisha fukwe za Tanzania na kutumia takataka za plastiki," alisema.

Aidha, Balozi alisema kuwa mradi huu unadhihirisha dhamira ya dhati ya Serikali ya Marekani kusaidia elimu nchini Tanzania.

"Shule zinapokuwa salama, safi na zenye vifaa vyote vinavyohitajika wanafunzi hujifunza vyema zaidi.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali ya Marekani imewekeza Dola za Kimarekani milioni 67.1 katika mfumo wa elimu ya msingi wa Tanzania kwa kusaidia kuandaliwa kwa mtaala unaozingatia umri kufundisha kuandika, kusoma na kuhesabu kwa darasa la kwanza hadi la nne na kuwafikia wanafunzi 825,000 na takriban walimu 10,000 katika wilaya 42 nchini.



Mafundi wakipiga plasta madarasa mapya ya Shule ya Msingi Etaro, wilayani Musoma, mkoani Mara juzi, yanayojengwa kwa nguvu na wananchi shuleni hapo, ambapo ina madarasa tisa, lakini mahitaji halisi ni 23. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Waziri aagiza kigogo RUWASA afukuzwe

**Na Paul Mabeja,** KONGWA

WAZIRI wa Maji, Jumaa Aweso, ameagiza kufukuzwa kazi kwa aliyekuwa Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Wilaya ya Kongwa, Hebert Kijazi, kutokana na kutumia Sh. milioni 609 kutekeleza mradi wa maji yasiyofaa kwa matumizi ya binadamu.

Mradi huo umetekelezwa Mkoka wilayani humo ambapo kwa sasa Kijazi ni Meneja wa RUWASA Wilaya ya Hanang mkoani Manyara. Hatua hiyo ya Aweso imetokana na malalamiko kutoka kwa wananchi na majibu ya maabara yaliyotolewa baada ya kupima maji hayo na kuonyesha uwapo wa chumvi nyingi na hivyo kutofaa kwa matumizi ya binadamu.

Wananchi hao walimweleza waziri huyo kuwa maji hayo yanasababisha ugali usiive, nguo kubaki na madoa na kutumia sabuni nyingi wakati wa kufua.

Akizungumza na wananchi hao, Aweso alisema mradi huo ulifadhiliwa na Benki ya Dunia na kwamba Kijazi ndiye alikuwa msimazi wa mradi huo akiwakilisha serikali kwa upande wa Wilaya ya Kongwa.

Waziri Aweso alisema kwa mujibu wa ripoti iliyopo iliyoandaliwa na wataalamu wa maji, maji katika mradi huo yalikuwa hayafai kwa matumizi ya binadamu lakini bado mradi huo uliendelea kutekelezwa.

"Ripoti iliyotolewa mara baada ya maji haya kupimwa katika chanzo, ilibanisha kuwa hayafai kwa matumizi ya binadamu lakini wao kutokana na kutaka kupiga fedha hizo waliendelea kutekeleza bila kujali afya za wananchi hawa," alisema Aweso.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Aweso alimwagiza Katibu Mkuu, Anthony Sanga, kumfukuza kazi mtumishi huo.

"Katibu Mkuu apatiwe salamu huyu mhandisi anatakiwa kuondolewa mapema, watu kama hawa hawana nafasi katika Wizara hii ya Maji,"alisisitiza Aweso.

Aliwaagiza Meneja wa RUWASA Mkoa wa Dodoma pamoja Kongwa kumwandikia maelezo kwa nini asiwafukuze kazi kutokana na kumdanganya awapatie kiasi cha Sh. milioni 356 kwa ajili ya ukarabati wa mradi huo ambao maji yake hayafai.

"Ninaagiza hadi Jumatatu wiki ijayo mnililete ofisini kwangu maelezo kwa nini nisiwafukuze kazi kwa kunidanganya ili nitoe kiasi hicho cha fedha kwenye mradi ambao umekula Sh. milioni 609 bila kuwa na tija yoyote kwa wananchi," aliagiza.

Aliwaonya wahandisi ambao wamekuwa na tabia ya kuchezea miradi ya maji, akiwataka kuacha tabia hiyo kwa kuwa hakuna atakayeachwa salama.

Alisema wizara hiyo imetoa kiasi cha Sh. milioni 341 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika mji wa Kongwa ambayo itasadia kupeleka maji katika tangi la lita milioni moja ili kupunguza adha ya upatikaji wa huduma hiyo. Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, Dk. Suleiman Serela, aliishukuru serikali kwa jitihada zinazaofanywa ili kutatulia kero ya upatikanaji maji safi na salama.

# Madereva 51 wafutiwa leseni

**Na Moshi Lusonzo**

MADEREVA 51 wamefutiwa leseni baada ya kubainika kuendesha magari kwa mwendokasi na kukiuka sheria za barabarani.

Kamanda wa Kikosi cha Usalama Barabarani, SACP Broad Mtafungwa, alisema hayo wakati wa maadhimisho ya kimataifa ya usalama barabarani chini ya Umoja wa Mataifa, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam, jana.

Mtafungwa, alisema madereva wote waliofutiwa leseni zao hataruhusiwa kufanya kazi hiyo, hadi watakaporudi darasani kusoma upya na kuthibitishwa na mamlaka husika kama wana weledi na umakini wa kuendesha chombo cha moto.

"Madereva wote tuliowafutia leseni zao endapo wataingia barabarani tutawakamata na kuwafungulia mashtaka kwa sababu wao hawana sifa na kama wakitaka kurudia kazi hiyo lazima waende tena darasani," alisema SACP Mtafungwa.

Aidha, alisema adhabu ya kufuta leseni inakuwa ya mwisho kama mhusika atakuwa anavunja sheria mara kwa mara.

Alitaja hatua zingine wanazochukua kupunguza ajali ni pamoja na kutoza faini na kutoa elimu ya moja kwa moja kwa madereva.

Alikipongeza Chama cha Wamiliki wa Magari ya Michezo (AAT), kutoa elimu ya usalama barabarani katika ngazi ya shule za msingi na kuwajengea watoto ufahamu wa matumizi ya barabara.

Ofisa Mtendaji wa AAT, Yusuf Ghor, alisema maadhimisho hayo yanayobeba kaulimbiu ya 'Mitaa kwa Maisha', ina lengo la kuhamasisha madereva kupunguza mwendo kasi hadi kilomita 30 kwa saa katika maeneo yenye wingi wa watu hasa shule, hospitali na makazi ya watu.

Alisema katika mpango wa utoaji wa elimu hiyo, jumla ya wanafunzi wa shule za msingi 5,000, walimu 2,500 na waendesha bodaboda 550 wamenufaika.

"Nia yetu ni kuona watoto wanakuwa salama zaidi wanapokwenda na kurudi shuleni," alisema Ghor.

Mwenyekiti wa Wamiliki pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam, Philipo Mtoro, alisema wanaishukuru AAT kwa kuwapatia msaada wa kofia ngumu 850 kwa madereva wa bodaboda.

Alisema kutokana na elimu ya usalama barabarani waliyopatiwa watakuwa mabalozi wazuri watakapokwenda mitaani na kupunguza madhara yanayotokana na uzembe.

# Kortini tuhuma hujuma bomba la TPA

**Na Hellen Mwango**

WATU wanne wakazi wa Kigamboni, mkoani Dar es Salaam, wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuingilia miundombinu na kuharibu bomba la mafuta aina ya dizeli mali Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Washtakiwa hao ni, Issa Hussein (57), mfanyabiashara, mkazi wa Kigamboni Darajani, Mechuma Juma (45) mvuvi, mkazi wa Kigamboni Mfinanga, Radhamani Kondo (35), mtunza fedha, mkazi Kigamboni na Joseph Fundi (60), mlinzi wote walisomewa mashtaka yao katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ritta Tarimo, ilisikiliza mashtaka dhidi ya washtakiwa hao. Wakili wa Serikali Mwandamizi, Wankyo Saimon, alidai shtaka la kwanza washtakiwa wote wanatuhumiwa katika tarehe zisizo fahamika, Januari, mwaka huu, ndani ya Wilaya ya Kigamboni, Mkoa wa Dar es Salaam walikula njama ya kuharibu miundombinu.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa katika tarehe zisizofamika, Januari, mwaka huu, washtakiwa wakiwa eneo Flow Meter, waliingilia na kuharibu bomba la mafuta aina ya dizeli la TPA.

Ilidaiwa kuwa, baada ya kufanya uharibifu huo washtakiwa waliisababishia TPA hasara ya Sh. 1,433,500.

Hata hivyo, washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa sababu mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi ya Uhujumu Uchumi. Baada ya kuwasomea washtakiwa mashtaka, alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo haujakamilika na kuomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Aidha, alidai kuwa upande wa Jamhuri hauna pingamizi la dhamana dhidi ya washtakiwa.

Hakimu Tarimo, aliwataka washtakiwa kuwa na wadhamini wawili kila mmoja, wawe wakazi wa Dar es Salaam, watakaotia saini hati ya dhamana ya Shilingi milioni nne.

Sharti jingine alisema washtakiwa wasitoke nje ya Mkoa wa Dar es Salaam bila kibali cha mahakama.

Washtakiwa wawili, wameachiwa kwa dhamana baada ya kutimiza masharti hayo.

Kesi hiyo, imeahirishwa mpaka Juni 17, mwa huu kwa ajili yakutajwa na kuangalia hatua ya upelelezi ulipofikia.



Wasamaria wema wakiwatoa abiria kwenye bajaj iliyopata ajali, eneo la Ukonga Mombasa, jijini Dar es Salaam, juzi. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

# Serikali yapiga marufuku usafirishaji wa nguruwe

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

NGURUWE 12 wamethibitika kufa kutokana na homa ya nguruwe Manispaa ya Morogoro na serikali imepiga marufuku usafirishaji wa wanyama hao na nyama yake kutoka nje ya mkoa huo.

Aidha, kata tano kati ya 29 za Manispaa ya Morogoro zimethibitika kuathiriwa na ugonjwa huo.

Ofisa Mifugo wa Manispaa ya Morogoro, Dk. Petro Lema, alithibitisha hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuwa ugonjwa huo hauna madhara kwa binadamu atakekula nyama ya nguruwe aliyeathiriwa.

Alisema walipata taarifa ya kuibuka kwa ugonjwa huo Juni 2 na kuchukua sampuli kuzipeleka maabara ya chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na kubaini kuwapo kwa vimelea vya ugonjwa huo kwa nguruwe waliokufa katika kata za Kingolwira, Tungi, Kichangani, Boma na Kilakala.

Dk. Lema alisema uchunguzi wa awali wamebaini kuwa ugonjwa huo kutokea mkoani Dodoma na Manispaa ya Morogoro ulianzia kata ya Kingolwira na idara ya mifugo kwa kushirikiana na jeshi la polisi tayari wameshaweka vizuizi katika mpaka wa barabara ya Iringa, Dodoma na Dar es salaam ili kuzuia wafanyabiashara kuingiza au kutoa wanyama hao.

Alisema wanaokula nyama hiyo kwenye vibanda, mabucha na baa hawaruhusiwi kubeba mabaki kupelekea mifugo nyumbani ili kuepuka ugonjwa huo kusambaa.

"Tumeendelea kutoa elimu kwa makundi mbalimbali wakiwamo wauzaji wa kitoweo cha nguruwe, wafugaji na wauzaji chakula cha mifugo, ugonjwa huu unasababishwa na kirusi na hautibiki," alisema.

Pia, alisema atakayekiuka masharti atachukuliwa hatua ikiwamo kutozwa faini ya Sh. 200,000 na watakaobainika kuwa na nyama hiyo bila mihuri, nyama itateketezwa.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **GADAU AUCTION MART AND COMPANY LTD, MASE INTERNATIONAL LTD** na **MAK RECOVERIESLTD** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD,** kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
|---|---|---|---|
| 1 | Charles Ntyuka Mhoja | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Majengo Mapya - Morogoro Mjini |
| 2 | Alex Mtesigwa Bulenga | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kihonda – Barabara ya Mazimbu - Morogoro |
| 3 | Juma M. Mushi | Gari aina ya Nissan Caravan Na ya usajili T765 DLC | Morogoro Mjini |
| | MAK RECOVERIES LTD | | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 4 | Godfrey Salieli Mtui | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Chumbageni - Tanga Mjini |
| 5 | Salimu Abdallah Bori | Lori aina ya Daf Tractor Multicolor yenye namba za usajili T 396 CLS na Trailer Multicolor lenye namba za usajili T 157 BKS | Duga Mwembeni - Tanga Mjini |
| 6 | Halima Omar Hoza | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Amboni Mafuriko,Tanga Mjini |
| 7 | Elizabeth Mchomvu | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mpwapwa –Dodoma |
| 8 | Ruth D Sakala | Samani za nyumbani | Kwa mama John - Mbeya |
| 9 | Emmanuel V Ngonde | Nyumba yenye mkataba wa mauziino na Mitsubishi canter yenye namba ya usajili T350 ABB | Mwakapangala Mbalizi – Mbeya |
| 10 | Fidea A Mbogela | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mwanjelwa - Mbeya |
| 11 | Mansour Athuman Mbarouk | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Isyesye - Mbeya |
| 12 | Janken A Mwalyego | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Ihuhu – Mbeya MJINI |
| 13 | Cecilia J Sintala | Samani za biashara na samani za nyumbani | Mbeya |
| 14 | Neema Hassan Ambonisye | Nyumba yenye mkataba wa mauzino | Mayombo - Iwambi |
| 15 | Burton W Chombe | Nyumba iliyoko kiwanja numba 219, kitalu D", Mbalizi mbeya | Mbalizi - Mbeya |
| | MASE INTERNATIONAL LTD | | |
| | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 16 | Diana Stevene Kitara | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kekiberi - Tarime |
| 17 | Thomas Mhonja Mayalla | Nyumba yenye hati, kiwanja namba 149, Kitalu E' Majengo kahama mjini | Majengo - Kahama Mjini |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo, mahali ilipo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipa ndani ya siku kumi na nne (14) toka tarehe ya mnada, kinyume na hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (Transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

Mkurugenzi Mtendaji
Gadau Auction Mart and Company Limited
P.o.box 40855
Dar es Salaam

Na
Mkurugenzi Mtendaji,
Mack Recoveries Ltd
0715 375475/ 0783224965
0716 35 3650/0763 481 798

Na
Mkurugenzi mtendaji,
Mase international Ltd
P.O. Box 6797
Mwanza

Na
Finca Microfinance Bank Ltd
P.O. Box 78783
Namba:0768790399, 0754774949

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wadau wa soka msichafuane kuelekea Uchaguzi Mkuu TFF

**HIVI** karibuni Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), ambalo kwa sasa liko chini ya Rais, Wallace Karia, limetangaza litafanya Mkutano Mkuu wa mwaka ifikapo Agosti 7, mwaka huu.

Moja ya ajenda katika mkutano huo wa mwaka ni Uchaguzi Mkuu wa kuweka viongozi wapya watakaokaa madarakani kwa muda wa miaka minne kama katiba ya shirikisho hilo inavyoelekeza.

Viongozi watakaochaguliwa katika mkutano huo, ndio watakuwa na dhamana ya kusimamia shughuli zote za mpira wa miguu hapa Tanzania kwa awamu nyingine ya miaka minne.

Hata hivyo, bado mchakato rasmi wa uchaguzi huo haujaanza na wadau wenye nia ya kugombea nafasi mbalimbali za uongozi hawajajulikana, ingawa baadhi yao wameanza kuonyesha nia.

Kuelekea uchaguzi tayari zimeanza kampeni chafu dhidi ya viongozi walioko madarakani na wengine ambao wanaonekana wana mpango wa kuweka nia.

Nipashe inawakumbusha wadau wa soka kuepuka kampeni chafu kuelekea kipindi hichi cha uchaguzi mkuu kwa sababu nyumba itakayojengwa ni moja na kubwa ni kuangalia maslahi na maendeleo ya soka hapa Tanzania.

Si vyema kipindi hichi kuona au kusikia wadau wakifanya kampeni chafu dhidi ya wapinzani wao au viongozi walioko madarakani kwa lengo la kuwaharibia na hivyo kuwashawishi wapira kura kufanya uamuzi ambao mwisho wa siku utawaumiza Watanzania.

Ili kufikia malengo yaliyowekwa na TFF ambayo ni kuona soka la Tanzania linazidi kuimarika kuanzia kwenye Ligi Kuu Bara, Timu za Taifa na wawakilishi wake kwenye mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika wanafanya vyema, ni lazima kuongeza umakini wa kuchagua watu watakaoupeleka mbele mpira wetu.

Kukosoa viongozi walioko madarakani ili wasichaguliwe tena si dhambi, ila itakuwa dhambi pale watakapopakwa 'matope' kwa mambo ambayo hawajayafanya lakini pia wadau hao hao wakikaa kimya kwa kutowasifia kwa mazuri waliyoyafanya ili tu wasionekane wema kwa taifa lao.

Tunaamini wadau wenye nia ya kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi mkuu ujao wanaweza kutumia mbinu mbalimbali kujinadi kwa kuandaa sera bora na kuacha kuwachafua wenzao kwa sababu wajumbe wa mkutano mkuu wanafahamu wapi wanapaswa kupeleka kura zao za ndio.

Wakati uchaguzi huo ukikaribia na msimu wa Ligi Kuu Tanzania Bara ukielekea ukingoni, baadhi ya timu ambazo zimekuwa na matokeo ya kusuasua zimeanza kutoa madai kwamba zinaonewa na viongozi walioko madarakani na wanafahamu kufanya hivi kuelekea kwenye uchaguzi kutawapunguzia imani kwa wajumbe wao.


Waswahili wanasema kizuri kinajiuza na kibaya kinajitembeza, naamini kila mdau anatakiwa kuacha mazuri aliyofanya na si kutumia maneno ya uongo kuwachafua wengine, dunia ya sasa ni ndogo na kila mmoja analofanya linaonekana tofauti na ilipokuwa miaka ya nyuma.

Pia tunawakumbusha wadau wa soka kokote nchini kujitokeza kusaidia maendeleo ya mchezo huo, kukosoa au kutoa michango ya maendeleo kwa wakati wote na haya yasitokee kipindi cha kuelekea uchaguzi.

Tunaamini viongozi ambao wanataka kuwania nafasi za uongozi katika uchaguzi huo utakaofanyika jijini Tanga, waweke mbele maslahi ya nchi huku wakiamini wana deni la kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zinazoogopewa kila inaposhiriki mashindano ya kimataifa.

Pia tunawakumbusha viongozi wa klabu na vyama vya mikoa kila mmoja wafanye majukumu yao vyema na kamwe wasijifiche kwenye kivuli cha mafanikio au upungufu ya TFF.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kiongozi ni mtu mwenye...

Na Barnabas Maro

**KIONGOZI** ni mtu mwenye madaraka ya kuelekeza watu wengine; msimamizi wa jambo linalofanywa na watu. Pia ni kitu kinachosaidia kuonyesha au kuelekeza; mwongozo.

Kwa hiyo 'Uongozi' ni dhamana ya kusimamia jambo kwenye taasisi au mahali penginepo. Ni madaraka anayopewa mtu ya kusimamia au kuongoza shughuli. "Ongoza" ni kuwa mbele ili kuonyesha mwelekeo fulani; simamia shughuli na onyesha jinsi ya kufanya jambo; elekeza.

Je, wanachama na mashabiki wa timu zetu za kandanda wanatambua hayo? Au wanachotaka ni ushindi tu bila kujua kama wachezaji na benchi zima la ufundi wanalipwa kila mwisho wa mwezi kama ilivyo kawaida ya waajiriwa?

Aidha wanajua jinsi fedha zinazopatikana michezoni zinavyotumiwa kwa manufaa ya vilabu vyao? Kama sio matajiri ndio wanaotoa kila kitu kama fedha za usajili wa wachezaji na mishahara yao hali ya vilabu vyetu ingekuwaje?

Matajiri ndio wanaofanya kila kitu kwenye vilabu vyetu. Kwani wao hawataki faida ya fedha wanazotoa vilabuni? Je, viongozi wa vilabu hawashiriki kwenye ulaji (wengine huita ('kupiga fedha') za vilabu vyao?

Hakuna tajiri yeyote ulimwenguni anayetoa fedha zake kwa klabu ya kandanda kusafirisha timu kwenda kucheza nchi za nje kisha asijue jinsi ya kurejesha fedha zake. Je, viongozi wa vilabu hawajui hilo au wanafurahia kunufaika wao kwa namna fulani, hivyo wanatulia tuli (bila ya kutikisika) bila kuhoji? Matajiri 'wanaozisaidia' vilabu vya kandanda humu nchini wana yao wanayopata ilhali wanachama huwashangilia na kuwasifu kumbe "kikulacho kinguoni mwako." Maana yake kikulacho huwa ndani ya nguo yako uliyoivaa. Methali hii yatukumbusha kuwa mtu anayeweza kutudhuru ni yule anayetufahamu vizuri. Mathalani anayeweza kutuhasiri (kitendo cha kumtia mtu hasara) ni rafiki yako au jamaa wa karibu!

Hebu tujiulize, kwa mfano, tangu mwaka 1935 ilipoundwa Yanga na mwaka uliofuata (1936) ilipoundwa Sundarland ambayo sasa yaitwa Simba, vilabu hivyo kongwe vimekuwa na maendeleo gani ya maana na ya kujivunia?

Mafanikio yao ni moja kuifunga nyingine na wanachama na mashabiki kutamba mitaani. Tena wengi wanaozishangilia Yanga na Simba sio wanachama bali ni mashabiki tu! Kumbe leo wanaweza kuwa Yanga, kesho wakawa Simba au mashabiki wa Simba kuishabikia Yanga wanapoona Simba inakwenda arijojo yaani hali ya kupotea; hali ya kupoteza mwelekeo.

Kwa hali ilivyo, Yanga na Simba, sasa sidhani kama kuna wanachama au mashabiki wanaoweza kukuonyesha jambo au ufanisi, yaani hali ya jambo kutekelezwa kama ilivyotarajiwa. Jaribu kujiuliza tangu miaka ya 1935 na 1936 zilipoundwa Yanga na Simba timu hizo zina maendeleo gani ya maana yaliyofanywa na viongozi wao!

Kwa nini wanaogombea nafasi za uongozi hutumia mbinu mbalimbali ili wachaguliwe? Wapo wanaotumia fedha kama rushwa ili wachaguliwe wana maana gani zaidi ya kula hela za vilabu? Baadhi yao wamejenga kupitia hela za vilabu vyao! Kumbe wajinga ndio waliwao!

Hivi karibuni Yanga walifiwa na mwanachama wao ambaye ndiye aliyekuwa kashikilia hati ya nyumba ya Yanga pale Jangwani. Tangu alipokuwa hai ni kiongozi yupi wa Yanga aliyejitahidi kujua ilipo hati ile? Kama aliuliza kutaka kujua ilipo alifanya juhudi gani kurejesha hati hiyo klabuni? Kwa nini hati ya nyumba ikae kwa mwanachama badala ya kuwa klabuni au benki?

Kumbe hati ya jengo la Yanga pale Jangwani ingeweza kutumiwa kuomba mkopo benki ili kujenga jengo la maana pale kwenye makutano ya barabara za Mafia na Nyamwezi kilipo 'kibanda' ambacho zamani ndicho kilikuwa makao makuu kabla ya jengo la ghorofa mbili pale Jangwani.

Ina maana baada ya aliyekuwa mwenyekiti wa Yanga wakati ule hakuna kiongozi yeyote wa Yanga aliyejibidisha kujua hati ya jengo ilipo? Walikuwa wakikabidhiana nini bila hati ya kiwanja? Kwa nini walinyamaza tu bila kufuatilia kwa bidii hati ile? Kadri miaka inavyopita ndivyo gharama za ujenzi zinavyozidi. Ukimya wa viongozi wote waliopita pale baada ya marehemu Mangara hawakuona umuhimu wa hati ya jengo lao?

Enzi za uongozi wa Mangara (Mungu amrehemu) Yanga ilikuwa tajiri hata gazeti la Daily Nation la Kenya kuandika kuwa klabu hiyo ndio tajiri kuliko timu zote za Afrika Mashariki. Yanga ilikuwa na mabasi matatu (mawili makubwa na moja dogo) na gari la mwalimu. Leo ina magari mangapi iliyonunua?

Yanga iliialika timu maarufu ya Brazil aliyokuwa akicheza mchezaji maarufu duniani, Pele. Wakati huo Yanga iliandaa kanga zilizoandikwa "Pele na Santos wageni wa Yanga" na kuuzwa kwa wanachama na mashabiki. Hata hivyo Pele na Santos yake hawakuja nchini kutokana na mipango waliyokuwa nayo kwao, ingawa mwanzo walikubali kuja Dar es Salaam. Je, viongozi waliofuata baada ya Mangara hawana cha kuiga kwa yale yaliyofanywa na marehemu huyo ili kuiletea Yanga maendeleo?

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## HABARI PICHANI

# WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI, BALOZI LIBERATA MULAMULA ATEMBELEA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Liberata Mulamula (katikati), akizungumza alipotembelea chumba cha habari cha kampuni ya The Guardian Ltd (TGL) inayochapisha magazeti ya Nipashe na The Guardian, Mikocheni, mkoani Dar es Salaam jana. Wengine ni Mhariri Mtendaji wa gazeti la Nipashe, Beatrice Bandawe (kushoto), Mkurugenzi wa TGL, Joyce Luhanga (wa pili kushoto), Meneja Rasilimali Watu Mwandamizi, Ayoub Semvua (wa pili kulia) na (kulia) ni Meneja wa Sheria na Rasilimali Watu, Emmanuel Matondo. **PICHA ZOTE: MIRAJI MSALA**



Meneja wa Uchapishaji wa TGL, Balasubramaniyan Venkadachalam (kushoto), akitoa maelezo kwa Balozi Liberata Mulamula alipotembelea kiwanda hicho.




Balozi Liberata Mulamula (kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Msemaji wa maswala ya wanawake wa EATV/EA Redio, Maryam Kitosi, katika studio za EA Radio.



Balozi Mulamula akifurahia jambo na Mkurugenzi Msaidizi wa Redio One, Bahati Alex (katikati) na Mtangazaji wa Capital Redio, alipotembeles studio za redio hiyo.



Mkurugenzi Msaidizi wa Capital Redio, Abdallah Mwaipaya, akifafanua jambo kwa Balozi Mulamula katika studio za Redio One.




Mkurugenzi wa Vipindi wa ITV, Pius Paul, akitoa maelezo kwa Balozi Liberata Mulamula, alipotembelea chumba cha kusomea taarifa ya habari cha televisheni hiyo.

## Mradi wa maji Tabora waiva

MBUNGE wa Bukene (CCM), Selemani Zedi amehoji hatua zilizofikiwa na serikali katika mradi wa maji kutoka Nzega mjini hadi Bukene.

Zedi alisema bungeni jana kuwa mradi huo utanufaisha wananchi wa vijiji 20 na vitongoji zaidi ya 100.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Maji, Maryprisca Mahundi, alisema katika mwaka wa fedha 2020/21 serikali imekamilisha kazi ya usanifu wa mradi wa kutoa maji katika tanki la Ushirika mjini Nzega kwa ajili ya kuhudumia watu zaidi ya 79,485 katika vijiji 20 na vitongoji vyake.

"Katika mwaka wa fedha 2021/22 kiasi cha fedha Sh. bilioni mbili kimetengwa na utekelezaji wa mradi huu utaanza, ambapo utahusisha kulaza mabomba ya kusambaza maji umbali wa Km 176," alisema.

Pia, alisema kujenga matanki matano ya kuhifadhi maji ya ujazo wa lita 100,000, lita 150,000, lita 250,000 na lita 300,000 na kujenga vituo vya kuchotea maji 83.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# Wahamiaji 1,000 wakamatwa

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema ndani ya miezi mitatu iliyopita wamekamatwa wahamiaji zaidi ya 1,000 nchini.

Simbachawene aliyasema hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Kigoma Mjini (CCM), Kilumbe Ng'enda.

Katika swali lake, Ng'enda alisema kiwango cha usumbufu wa wananchi Mkoa wa Kigoma kimepita kiasi na kuhoji kuna jambo lipi jipya linalosababisha kwa sasa kuwe na misako ambayo inasumbua raia waliokaa kwenye mkoa huo.

"Msingi wa kukua kwa tatizo hili ni wizara kuchelewa vitambulisho vya NIDA kwa wananchi halali wa Mkoa wa Kigoma. Ni lini serikali itakamilisha utoaji wa vitambulisho hivyo na ikiwezekana misako hiyo isimame hadi vitambulisho vipatikane?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri Simbachawene alisema idadi hiyo ni kubwa na si rahisi isifanyike doria na msako wa wahamiaji haramu unafanyika mikoa yote nchini.

"Kupewa kitambulisho cha uraia siyo mwarobaini wa kuonyesha kuwa wewe kuhusu uhalisia na uhalali wa uraia wako, sheria hizi ni mbili tofauti; kuna sheria ya uraia na ya uingiaji nchini na sheria ya vitambulisho vya taifa, zote hizi zinashughulikia mambo mawili tofauti," alisema.

Waziri huyo alisema katika vitambulisho hivyo kuna madaraja tofauti na wanapewa hata wakazi wasio raia na si kwamba mtu akipewa kitambulisho hataulizwa kuhusu uraia wake. "Hivi sasa kuna operesheni imeanza Mei Mosi na itaisha Mei 15, mwaka huu kwa mikoa yote ya Tanzania," alisema.

Waziri huyo alisema kiwango cha usumbufu katika kusimamia Sheria ya Uhamiaji kifungu cha 12 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2016, Idara ya Uhamiaji imepewa jukumu la kufanya msako na upekuzi ili kubaini nani raia na nani siyo raia, linafanyika kwa nchi nzima.

"Usumbufu unatokana na mkoa ulivyo na mipaka na majirani zetu ambao kumekuwa na shida kwenye nchi zao," alisema. Katika swali la msingi, Mbunge wa Kigoma Kaskazini (CCM), Assa Makanika, alihoji lini serikali itawasaidia wananchi wa Kigoma ambao wamekuwa wakikamatwa mara kwa mara kwa kuitwa wakimbizi nchini mwao.

Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Khamis Hamza Chilo, alisema alisema Idara ya Uhamiaji imepewa jukumu la kudhibiti, kusimamia na kufuatilia uingiaji, ukaaji na utokaji wa wageni nchini kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 12 (1) cha Sheria ya Uhamiaji Sura ya 54 na marejeo ya mwaka 2016.

"Katika kutimiza jukumu hilo, Idara ya Uhamiaji imekuwa ikifanya operesheni, doria na misako mbalimbali kwa lengo la kuwabaini wageni wanaoingia na kuishi nchini kinyume cha sheria na taratibu,"alisema.

Hata hivyo, alisema serikali imekuwa ikifanya mahojiano na uchunguzi wa kina ili kujiridhisha juu ya uraia wa watuhumiwa wanaokamatwa wakati wa operesheni husika na kwamba, Idara ya Uhamiaji katika kushughulikia masuala ya uraia huzingatia matakwa ya Sheria ya Uraia Sura ya 357 rejeo la mwaka 2002.



Waziri wa Maliasili na Utalii, Dk. Damas Ndumbaro (kushoto), akikabidhiwa hotuba ya makadirio ya bajeti ya wizara hiyo kwa mwaka 2021/2022 na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Mary Masanja, kabla ya kuiwasilisha bungeni jijini Dodoma jana. Kulia ni Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Inocent Bashungwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tatizo la ajira laundiwa mikakati minane kitaifa

SERIKALI imetaja mikakati minane inayofanywa katika kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wanapomaliza vyuo vikuu.

Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia watu wenye ulemavu, Ummy Nderiananga, alianika mikakati hiyo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Musoma Mjini (CCM), Vedastus Mathayo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mkakati gani mahususi wa kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana wanapohitimu vyuo vikuu.

"Je, ni kwa nini vijana hao wasitumie vyeti vyao kama dhamana kupata mikopo ili wajishughulishe na shughuli mbalimbali za kiuchumi?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Nderiananga alisema serikali imeandaa mkakati wa kitaifa wa kukuza fursa za ajira ambao unatoa maelekezo kwa sekta zote za kiuchumi ya namna ya sekta hizo zinavyopaswa kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji ili wawekeze na kuzalisha fursa za ajira za kutosha.

Alitaja mikakati mingine ni serikali kuanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya uzoefu wa kazi kwa wahitimu.

"Katika kipindi cha miaka mitatu jumla ya wahitimu 5,975 wamewezeshwa kupata mafunzo ya uzoefu wa kazi katika taasisi mbalimbali za umma na binafsi ikiwa ni mkakati wa kuondoa kikwazo cha uzoefu kwa vijana wanapotafuta kazi," alisema.

Naibu waziri huyo alisema serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya ufundi na stadi katika fani mbalimbali kwa vijana wakiwamo wahitimu wa elimu ya juu ambapo katika kipindi cha miaka tatu, jumla ya vijana 28,941 wamepatiwa mafunzo ya ujuzi na stadi za kazi kupitia mafunzo ya uanagenzi. "Serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo na kurasimisha ujuzi uliopatikana nje ya mfumo usio rasmi wa mafunzo kwa lengo la kuwawezesha vijana kuajiriwa au kujiajiri na pia kujiendeleza kiujuzi katika taasisi mbalimbali za mafunzo," alisema.

Vilevile, alisema serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya mafunzo ya kilimo cha kisasa kwa vijana wakiwamo wahitimu wa elimu ya juu kupitia teknolojia ya kitalu nyumba. "Serikali imeanzisha na kutekeleza programu ya vijana kufanya mafunzo ya uzoefu wa kazi katika sekta ya kilimo kwa kuwapeleka katika nchi ambazo zimepiga hatua katika kilimo ambapo katika mwaka ulipita tumegharamia vijana 136 kuhudhuria mafunzo ya kilimo cha kisasa Israel," alisema.

Aliongeza kuwa serikali imeendelea na mkakati wa pamoja wa ajira kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, Utumishi na Wizara nyingine na hasa kupitia miradi ya maendeleo.

"Vilevile, serikali imeanza kufanya utafiti kuhusu hali ya ajira nchini," alisema.

Hata hivyo, alisema serikali inapokea ushauri wa kutumia vyeti vya uhitimu mafunzo kama dhamana ya mikopo kwa vijana na inakwenda kufanyia kazi.

"Serikali imeendelea kuboresha huduma ya utoaji mikopo kwa vijana kupitia mifuko na program mbalimbali za uwezeshaji wananchi kiuchumi," alisema.



# Matatani kwa kushindwa kusafisha mashamba

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, amemwagiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino kuwaondoa wamiliki 86 ambao wamekaidi kusafisha maeneo yao kwenye shamba la ushirika la kilimo cha zabibu la Chabuma.

Shamba hilo lina ukubwa wa ekari 600 na kati yake, 300 zipo kwenye mfumo wa kisasa wa umwagiliaji.

Akizungumza katika ziara yake ya kukagua mchakato wa kulifufua shamba hilo lililoanzishwa mwaka 2008/09, Bashe alisema shamba hilo liliacha kuzalisha mwaka 2015 na alipolitembelea awali aliagiza wamiliki kusafisha maeneo yao ili kufufua kilimo hicho.

"Nilishatoa muda kila mtu asafishe shamba lake lakini kuna watu 86 hawakuonekana na hawajasafisha, pia kulikuwa kuna watu wakubwa wanamiliki mashamba.

"Ninaomba muwaondoe na mashamba hayo yagawiwe kwa wakulima wengine ambao wapo 'serious' kwa ajili ya kushirikiana katika safari ya kulifufua shamba hili.

"Ninawaambia atakayenizuia kuwaondoa watu hao labda awe ni Rais Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango na Waziri wangu wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, hao wanne tu ndiyo wanaoweza kunizuia kuwaondoa na hakuna mwingine maana uamuzi tulishafanya na tulishatoa muda, kama walifikiri tunafanya sanaa hapa..."" alionya.

Alisema awamu ya kwanza ya ufufuaji wa shamba hilo imekamilika na wanakwenda kuanza awamu ya pili.

Bashe alibainisha kuwa katika shamba hilo kulikuwa kuna visima vitatu vya maji ambavyo vilikuwa vinatoa maji lita 40,000 hadi 50,000 kwa saa na bwawa linahifadhi lita 41,000.

Alitoa siku 15 kuhakikisha kazi zote zinakamilika ili mradi huo uanze mwaka huu.

"Tulijiwekea lengo na wakulima hapa kwamba lazima mwaka huu shamba hili liamke na hatua za awali inatia moyo wakulima wameungana wanashinda wenyewe hapa shambani kwa kushirikiana na wataalamu wa Wizara ya Kilimo kwa ajili ya kulifufua.

"Na kama mnavyoona tayari bwawa limeshakuwa 'repaired' na maji yanaingia," alisema.

Bashe alisema kuwa baada ya shamba hilo kufufuliwa, watakaa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) ili watengeneze miundombinu itakayowawezesha wakulima kuuza mchuzi badala ya kuuza matunda ya zabibu ili kilimo chao kiwe na tija.

Awali, akitoa taarifa ya ukarabati wa bwawa na visima katika shamba hilo, Mhandisi wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji Mkoa wa Dodoma, Raphael Laizer, aliiomba serikali iwasaidie fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya kumalizia ukarabati.



Naibu Waziri wa Kilimo, Husein Bashe (kulia), akizungumza na wafanyakazi wa Chama cha Ushirika cha Chabuma Amcos Ltd na wafanyakazi wa Tume ya Umwagialiaji mkoa katika ziara ya kukagua ujenzi wa bwawa litakalotumika katika umwagiliaji wa mashamba ya kilimo cha zabibu jijini Dodoma jana. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Bunge laridhishwa ujenzi nyumba za NHC Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii imeridhishwa na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa nyumba 400 zinazojengwa mkoani Dodoma na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC).

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Dk. Aloyce Kwezi, alibainisha kuridhishwa na mradi huo juzi walipozuru kukagua ujenzi wa nyumba 300 katika eneo la Iyumbu na nyumba 100 wilayani Chamwino.

Alisema kamati imeridhishwa ujenzi wa nyumba hizo kwa viwango vinavyotakiwa na hatua hiyo ni darasa kwa wajenzi wengine.

"NHC inatarajia kujenga nyumba 1,000 na leo (juzi) tumetembelea 400, miradi hii kwa kweli inatakiwa kupongezwa ndiyo maana kamati yangu, imempongeza waziri kwa kazi nzuri na kuwapongeza watendaji wake, tumeona ubora wa miradi inayoendelea.

"Kwanza ni ubora lakini la pili miradi hii ni shamba darasa kwa wajenzi wabinafsi pamoja na wajenzi wengine ambao watapenda kwa ajili ya kuikuza Dodoma yetu, lakini tutafurahi zaidi kwa sababu lengo ni miradi ikamilike kwa wakati halafu wananchi waje wapate huduma," alisema.

Alisema wananchi wengi Dodoma ni wageni na wanahitaji nyumba lakini zinauzwa kwa gharama kubwa na kwamba mradi huo utatoa nafuu kwao.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, alisema nyumba hizo zitakopeshwa kwa wananchi wakiwamo wafanyakazi wa serikali.

"NHC inautumia mradi huu kama shamba darasa kuwafundisha 'Real Estate' namna bora ya kujenga nyumba imara lakini pia kumekuwa na udhaifu kwa wauzaji wa nyumba ambao wamekuwa wakifanya udanganyifu kwa kuwauzia nyumba matokeo yake wafanyakazi wanalipa kwa muda mrefu," alisema.

Waziri Lukuvi alisema serikali itamsaidia mnunuzi wa nyumba kupata mkopo benki kwa riba nafuu ambao hautakuwa mgumu kwake kuulipa.

Alisema mpango wa serikali ni kujenga nyumba katika kila eneo nchini.

"Sisi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa sekta ya nyumba tumeiteua Shirika la Nyumba kama kiongozi wa wajenzi wa nyumba hizi za makazi.

"Kwa kweli hatutaruhusu kununua nyumba zaidi ya moja na tutawajua tu hatutaki nyarubanya hapa kwamba ununue zote halafu upangishe watu wote, haiwezekani, Serikali imetoa fedha hizi ili mwananchi akopeshwe kwa gharama nafuu," alisema.

Mkurugenzi wa NHC, Dk. Maulidi Banyani, alisema dhamira yao ni kujenga miradi mingi nchini kwa kuwa kuna ardhi ipo ya kutosha.

"Sisi kama NHC yapo maeneo mbalimbali nchini tunadhamiria kujenga miradi ya namna hii, ili tuweze kufanikisha haya ni lazima tuwe na ardhi na sisi kwa hivi sasa tuna ardhi katika maeneo mbalimbali kwa mfano Mtwara, Mara na Lindi," alisema.

Alisema kwa Mkoa wa Dodoma wamefanya mazungumzo na Jiji la Dodoma na tayari wameshapata ardhi maeneo ya Mapinduzi na Mahoma kwa ajili ya awamu ya pili ya ujenzi wa nyumba maalum za viongozi.

"Kwa hiyo tumejiandaa na tunahakika kwamba miradi hii itaendelea kutekelezwa sehemu mbalimbali za nchi," alisema.

# Wataka lugha ya alama hospitalini

**Na Peter Mkwavila,** KONGWA

SERIKALI imeombwa kuwapatia elimu ya lugha ya alama watoa huduma za afya katika vituo vya afya na zahanati wilayani Kongwa, ili kuyahudumia na kuyatambua kwa usahihi makundi ya watu wenye ulemavu.

Rai hiyo ilitolewa jana na Tabibu wa Zahanati ya Mautya wilayani humo, Suzana Petro, alipozungumza kwa niaba ya watoa huduma za afya kwenye mafunzo ya utoaji huduma jumuishi za afya kwa watu wenye ulemavu yaliyofadhiliwa na taasisi isiyo ya kiserikali ya Foundation for Civil Society (FCS).

Alisema elimu ya lugha ya alama inahitajika kufundishwa kwa kuwa itawasaidia katika kuwahudumia na kuwatambua watu wenye ulemavu.

"Tunaiomba serikali kutupatia fursa hiyo ya mafunzo ya lugha ya alama ili kuwahudumia ipasavyo kama tunavyowahudumia watu wasio kuwa na ulemavu.

"Kwa mfano, mtu mwenye ulemavu hawezi kuongea na wala hasikii na anaongea kwa ishara tu, anapohitaji kuhudumiwa kwa upande wetu tunalazimika kuomba msaada wa wataalamu wa lugha ya alama ili tuweze kuwahudumia, suala ambalo hatuwatendei haki makundi hayo ya walemavu," alisema.

Vilevile, aliiomba serikali kufanya marekebisho ya miundombinu ya baadhi ya majengo ya vituo vya afya na zahanati kwa kuwa siyo rafiki kwa makundi hayo ya watu wenye ulemavu.

Katibu wa Shirikisho la Watu Wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Mkoa wa Dodoma, Justust Ng'wantalima, alisema kuwa bado kuna unyanyapaa na ubaguzi kwenye vituo vya afya na zahanati, hali ambayo inayowakatisha tamaa pindi wanapougua na kushindwa kupata huduma ya kiafya.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, aliwataka wahudumu wa afya na zahanati kuonyesha upendo kwa vitendo kwa watu wenye ulemavu pindi wanapowahudumia.

Alisema serikali inatambua watoa huduma za afya kwenye vituo na zahanati wengi hawana taaluma ya kutambua lugha hiyo ya alama hivyo wasiwakimbie bali wahudumieni kama ilivyo.





# Zanzibar kuanza na chanjo ya kipindupindu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema inakusudia kuanza kutoa chanjo ya kukabiliana na ugonjwa wa kipindupindu ambao ni miongoni mwa maradhi ya mripuko yanayosababisha vifo vingi kwa wakati mmoja.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Afya Ustawi wa jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, wakati akitoa taarifa kuhusu chanjo hiyo kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Alisema maandalizi yamekamilika ikiwamo kufanyika kwa utafiti kuhusu chanjo hiyo na madhara yake.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba Wizara ya Afya ipo katika mchakato wa kuanzisha chanjo kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu kwa wananchi wake wa Unguja na Pemba," alisema.

Alisema chanjo hiyo itafanyika katika baadhi ya maeneo ambayo ni hatarishi na miripuko ya ugonjwa wa kipindupindu mara kwa mara hujitokeza nchini na kusababisha vifo vya wananchi wengi.

Mazrui alisema maandalizi ya chanjo hiyo yanafanywa kwa ushirikiano na Shirika la Afya Duniani (WHO), ambao wapo tayari kutoa ushirikiano wa kitaalamu.



Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Hemed Suleiman Abdula, akiwaongoza Waumini wa dini ya kiislamu kuusalia mwili wa marehemu Wahida Yussuf, aliyefariki kwa ajali ya basi la Classic mkoani Shinyanga, kabla ya mazishi yake katika makaburi ya Mwanakwerekwe, Zanzibar juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Chuo cha Nkurumah mbioni kurudishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imesema imewasilisha serikalini mapendekezo ya kurudisha Chuo cha Ualimu Nkurumah ambacho kilikuwa kikitoa mafunzo ya cheti cha ualimu.

Waziri wa wizara hiyo, Simai Mohammed Said, alitoa kauli hiyo wakati akijibu swali alilouliza na Mwakilishi wa Jimbo la Nungwi, Abdalla Abasi Wadi, aliyetaka kujua wizara ina mpango gani wa kurudisha mafunzo ya cheti cha ualimu katika chuo hicho hasa ikizingatiwa kuwa Nkurumah ilikuwa chuo cha kwanza kutoa mafunzo hayo.

Alisema kwa sasa wizara inasubiri uamuzi wa serikali.

Aidha, alisema kwa sasa mafunzo ya cheti katika ngazi ya maandalizi na msingi yanaendelea kutolewa katika vyuo vya ualimu ambavyo ni Chuo cha Kiislam Unguja na Chuo cha Ualimu cha Kiislam Pemba.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwandaa walimu wenye sifa na uwezo wa kufundisha wanafunzi kwa ufanisi katika ngazi za maandalizi na msingi.

Waziri Simai alisema wizara yake inaimarisha mafunzo kayo ya kuwapatia wakufunzi mafunzo ya ufundishaji ya mara kwa mara.

Alisema wizara inaendelea na marekebisho ya mtaala wa ngazi hiyo ya ualimu kwa kuwa kukamilika kwa mtaala huo utasaidia kufikiwa kwa mahitaji halisi ya kupata walimu wenye sifa nzuri kama walivyokuwa wahitimu wa Chuo cha Ualimu Nkurumah.

# SMZ yafaidika na fedha za Diaspora

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar, imesema inafaidika kwa kiasi kikubwa na fedha zinazotolewa na Wazanzibari wanaoishi nje ya nchi Diaspora.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Mudrik Ramadhan Soraga, aliyasema hayo katika ukumbi wa Baraza la Wawakilishi Chukwani, wakati akijibu swali la nyongeza lililoulizwa na Mwakilishi wa Nafasi za Vijana Hudhaima Mbarak Tahir.

Mwakilishi huyo alitaka kujua fedha zinazotolewa na diaspora kuisaidia Zanzibar serikali inafaidika vipi na fedha hizo zinazotumwa kupitia benki na miamala mengine ya kifedha.

Alisema pia, zipo fedha zinazoingia katika jamii na kusaidia mambo mbalimbali ikiwamo ujenzi wa shule, huduma za maji na kurekebisha miundombinu ya barabara.

Kadhalika, Diaspora husaidia jamii kuwaletea watalaamu mbalimbali ikiwamo madaktari, walimu na mainjinia, na mchango wao ni mkubwa katika kuisaidia nchi yao.

"Tukumbuke kuwa Diaspora wana mtandao mkubwa duniani ikiwamo watu mashuhuri, wawekezaji, wasanii hivyo kama nchi inanufaika pia kwa mtandao huo kuleta wadau katika kushajihisha shughuli za maendeleo katika nchi," alisema.

Waziri huyo alisema ofisi yake inaendelea kuchukua jitihada mbalimbali katika kuwatambua wanadiaspora ili kuelewa walivyotawanyika kijografia, kijinsia, ujuzi na uzoefu walionao.

Hata hivyo, alisema ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar kupitia utafiti wa mapato na matumizi ya kaya 2019/2020, imewawezesha kufahamu takwimu za idadi ya kaya zinazopokea misaada na fedha kutoka kwa wanadiaspora waliokuwapo nje ya nchi.

Alisema utafiti umebaini kuwa Zanzibar ina kaya 49,136 zinazopokea misaada ya fedha kutoka kwa wanadiaspora.

Aidha, alisema kwa wilaya zote 11, Wilaya ya Magharibi 'A' inaongoza kwa kuwa na kaya 9,043 zinapokea misaada na fedha kutoka kwa wanadiaspora ikifuatiwa na Wilaya ya Mjini yenye kaya 8,5123 na Wilaya ya Kaskazini 'B' ambayo ina kaya 548.

Waziri Soraga, alibainisha kuwa ripoti hiyo inafafanua kuwa asilimia 42.4 ya misaada na fedha zinazoingia Zanzibar kutoka kwa wanadiaspora zinatokea Oman ikifuatiwa na Uingereza asilimia 14.9, Canada asilimia 4.7 na Ausralia asilimia 3.3.

Alisema asilimia 61.9 ya fedha na misaada inayotumwa na wanadiaspora wa Zanzibar inatumika katika matumizi ya kawaida ya kugharamia elimu na afya na ununuzi wa mavazi ya wanafamilia katika kaya na asilimia 19.4 pekee hutumika kwa kuweka akiba na kufungua biashara na vitega uchumi kwa wale wanaopokea misaada hiyo.

Alisema kwa sasa ofisi yake inaendelea kuwatafuta popote walipo ulimwenguni kwa lengo la kuwaunganisha na kuwashajihisha wanadiaspora wote wa Zanzibar.




## HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA DKT. DAMAS NDUMBARO (MB) WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022



# HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII, MHESHIMIWA DKT. DAMAS DANIEL NDUMBARO (MB.), WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**1.0 UTANGULIZI**

**1.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii, ninaomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021, pamoja na kujadili na kupitisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema, na kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii kwa mara ya kwanza nikiwa Waziri wa Maliasili na Utalii. Aidha, kwa namna ya pekee na kwa masikitiko makubwa naomba niungane na wenzangu kutoa pole kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; Mheshimiwa Job Yustino Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Prof. Ibrahim Hamis Juma, Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waheshimiwa Wabunge wote; Chama Cha Mapinduzi; na Watanzania wote kwa ujumla kwa kuondokewa na mpendwa wetu, Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Tano (5).

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** hakika uzalendo, uchapakazi na umahiri wake katika kuliongoza Taifa letu pamoja na mchango wake mkubwa katika kulinda, kutetea na kuimarisha shughuli za uhifadhi wa maliasili na uendelezaji utalii nchini, hautasahaulika kamwe na utaendelea kukumbukwa na kuenziwa daima. Miongozo na maelekezo yake yameiwezesha Wizara na Taifa kwa ujumla kupata mafanikio na kusonga mbele katika maeneo mbalimbali. Vilevile, natoa pole kwa Watanzania wenzangu kwa kuondokewa na Viongozi wengine Wakuu wakiwemo: Mheshimiwa Maalim Seif Sharif Hamad, aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na Mheshimiwa Balozi Mhandisi John William Herbert Kijazi, aliyekuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Sisi sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea, Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** naungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa salamu za pole kwako binafsi, Bunge lako Tukufu, wananchi na familia za marehemu kwa kuondokewa na Waheshimiwa Wabunge wafuatao: Mheshimiwa Mhandisi Atashasta Justus Nditiye aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Muhambwe; Mheshimiwa Khatib Said Haji aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar; na Mheshimiwa Martha Jachi Umbulla aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum, Mkoa wa Manyara. Vifo vya Wabunge hao vimeleta majonzi makubwa kwa Waheshimiwa Wabunge na Taifa kwa ujumla kutokana na kukosa michango yao muhimu katika utendaji wa Bunge letu. Aidha, natoa pole kwa ndugu, marafiki na watumishi wote wa Wizara kutokana na baadhi ya watumishi kupoteza maisha, na wengine kujeruhiwa wakiwa wanatekeleza majukumu ya uhifadhi wa maliasili. Vilevile, ninatoa pole kwa wananchi ambao wamepoteza maisha na waliopata madhara kutokana na wanyamapori wakali na waharibifu. Namuomba Mwenyezi Mungu awaponye majeruhi na azilaze roho za marehemu mahali pema peponi, Amina.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdori Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.) kwa kuendelea kuaminiwa kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; na Mheshimiwa Balozi Hussein Athman Kattanga kwa kuteuliwa kuwa Katibu Mkuu Kiongozi. Pia, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri wote kwa kuteuliwa kusimamia majukumu ya Sekta mbalimbali. Aidha, ninawapongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umahiri mkubwa.

**6.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa, niishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Aloyce Andrew Kwezi (Mb.) na Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Dkt. Pius Stephen Chaya (Mb.) kwa ushirikiano, maoni na ushauri wanaoendelea kutoa kwa Wizara. Maoni na ushauri wao umeendelea kuwa chachu ya mafanikio katika kuhifadhi na kusimamia matumizi endelevu ya maliasili, malikale na kuendeleza utalii. Wizara itaendelea kushirikiana kikamilifu na Kamati hii na Bunge lako kwa ujumla katika utekelezaji wa majukumu yake na utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika sekta.

**7.** ***Mheshimiwa Spika***, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kunipa dhamana ya kusimamia Wizara hii ambayo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa nchi yetu. Aidha, ninawashukuru viongozi wenzangu wa Wizara akiwemo Mheshimiwa Mary Francis Masanja (Mb.), Naibu Waziri; Dkt. Allan Herbert Kijazi, Katibu Mkuu; na Ndugu Ludovick James Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu; kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Vilevile, ninawashukuru Watendaji Wakuu na watumishi wa Wizara; na wadau wote wa Sekta ya Maliasili na Utalii kwa ushirikiano wanaoendelea kutupatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Pia, kwa namna ya kipekee ninaomba kuishukuru familia yangu ikiongozwa na mke wangu mpendwa Bibi Florah Ndumbaro na Wananchi wa Jimbo la Songea Mjini kwa kuendelea kuniunga mkono katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku.

**8.** ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya maelezo hayo ya utangulizi, ninaomba sasa kuwasilisha hotuba yangu ambayo imejikita katika Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara wa mwaka wa fedha 2021/2022.

**2.0 MCHANGO WA MALIASILI NA UTALII KATIKA UCHUMI NA VIWANDA**

**9.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imejaliwa kuwa na rasilimali nyingi za maliasili na malikale zenye mchango mkubwa katika uendelezaji utalii, ukuaji wa uchumi, ustawi wa jamii na uhifadhi wa mazingira. Mathalan, utalii huchangia wastani wa asilimia 17 ya Pato la Taifa; asilimia 25 ya fedha za kigeni na huzalisha ajira takriban milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja kwa mwaka. Kwa upande mwingine, sekta ya misitu na nyuki huchangia asilimia 3.5 ya Pato la Taifa; asilimia 5.9 ya mapato yatokanayo na biashara ya nje na ajira takriban milioni 4 kwa mwaka. Sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 90 ya nishati ya kupikia nchini kutokana na miti (mkaa na kuni). Kutokana na mchango huo, rasilimali hizo zitaendelezwa na kusimamiwa ipasavyo ili ziendelee kuchangia zaidi katika uchumi na maisha ya wananchi kwa ujumla.

**3.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2020/2021**

**3.1 UKUSANYAJI MADUHULI**

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ilikadiria kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 218.55** kutokana na vyanzo vinavyosimamiwa moja kwa moja na Wizara. Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2021, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 147.28** sawa na asilimia 67 ya lengo. Aidha, taasisi za Wizara ambazo makusanyo yake yanapitia TRA ambazo ni TANAPA, NCAA na TAWA ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 584.63.** Hadi mwishoni mwa mwezi Aprili 2021, Taasisi hizo zilikusanya jumla ya **Shilingi bilioni 89.57** sawa na asilimia 15 ya lengo la makusanyo. Kutofikiwa kwa malengo hayo kulisababishwa kwa kiasi kikubwa na uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19.

**3.2 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO**

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 114.59** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 69.57** zilikuwa za matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 45.02** zilikuwa za miradi ya maendeleo. Hadi mwezi Aprili 2021, Wizara ilipokea na kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 64.59** sawa na asilimia 56 ya bajeti iliyoidhinishwa. Fedha zilizopokelewa zinajumuisha **Shilingi bilioni 48.85** za matumizi ya kawaida na **Shilingi bilioni 15.74** za miradi ya maendeleo.

**3.3 MAFANIKIO**

**12.** ***Mheshimiwa Spika***, katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imepata mafanikio mbalimbali yakiwemo:

**(i) Kuboresha Miundombinu ya Utalii**

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imefanikiwa kuboresha miundombinu ya huduma za utalii katika maeneo yaliyohifadhiwa ambapo barabara zenye jumla ya urefu wa kilometa 73.4 zimejengwa na kilometa 8,599.8 zimekarabatiwa; kambi za kitalii na loji zenye jumla ya vitanda 670 zimejengwa; njia za utalii wa kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilometa 927 zimejengwa; na malazi ya kitalii ya gharama nafuu yenye jumla ya vitanda 105 yamejengwa. Katika hatua nyingine, Wizara imenunua kivuko cha *MV Rubondo Island* chenye ukubwa wa tani 25 ambacho kina uwezo wa kubeba magari manne (4) na watu 25 kwa wakati mmoja. Hatua hizi zitasaidia kuongeza idadi ya watalii na mapato zaidi kwa Serikali.

**(ii) Kuendelea kwa Shughuli za Utalii katika Kipindi cha COVID-19**

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea kupokea watalii licha ya uwepo wa mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 ambapo watalii 620,867 kwa mwaka 2020 walitembelea nchini ikilinganishwa na matarajio ya watalii 437,000 yaliyokadiriwa awali kwa kuzingatia uwepo wa ugonjwa huo, **sawa na asilimia 142 ya lengo**. Aidha, jumla ya watalii wa ndani 571,353 walitembelea vivutio mbalimbali vya utalii nchini. Mafanikio hayo yalitokana na mikakati mbalimbali ikiwemo kuandaliwa kwa Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii - SOPs katika kipindi cha COVID-19. Kwa upande mwingine, Tanzania imefanikiwa kuwa miongoni mwa nchi chache za Afrika zilizofanikiwa kupata Muhuri wa *Safe Travel* wa Baraza la Usafiri na Utalii Duniani (WTTC).

**(iii) Kuongezeka kwa Umaarufu wa Hifadhi za Tanzania Duniani**

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia jitihada za Wizara za kuboresha shughuli za uhifadhi na kutangaza utalii kwenye masoko mbalimbali, Tanzania imepata tuzo za kimataifa zifuatazo: Hifadhi ya Taifa Serengeti kuwa hifadhi bora barani Afrika, kuwa mshindi wa pili Afrika na wa 12 duniani kwa kuwa na idadi kubwa ya wafuatiliaji wa ukurasa wake katika mtandao wa kijamii wa *Instagram* kwa mwaka 2020. Hifadhi hii pia imetambuliwa na Gazeti Maarufu la Forbes la nchini Marekani kama kivutio cha pili (2) duniani miongoni mwa vivutio bora 21 vya kutembelewa mwaka 2021. Aidha, Hifadhi za Taifa Kilimanjaro, Serengeti na Tarangire zimeshinda tuzo ya *Traveler best of the best 2021*. Kwa upande mwingine, Kiwanja cha Ndege cha Msembe katika Hifadhi ya Taifa Ruaha kimefanikiwa kuwa kiwanja chenye mandhari nzuri zaidi Afrika kwa mwaka 2020. Sambamba na hilo, TANAPA imetangazwa kuwa mshindi wa kundi la dhahabu miongoni mwa washindi 51 kutoka nchi 39 duniani wa tuzo ya huduma za viwango kwa mwaka 2020.

**(iv) Kuendeleza Mazao Mapya ya Utalii**

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza wigo wa mazao ya utalii na kuvutia watalii, Wizara imefanikiwa kuendeleza mazao mbalimbali yakiwemo utalii ikolojia; utalii wa jiolojia; utalii wa faru; utalii wa kuona wanyamapori nyakati za usiku; utalii wa farasi; utalii wa kupiga makasia; na uvuvi wa kujiburudisha. Aidha, katika kuendeleza utalii wa malikale, Wizara imeanzisha makumbusho mpya katika eneo la Urithi wa Dunia la Kilwa Kisiwani. Sambamba na hilo, Wizara imefungua fursa za shughuli za utalii katika Ukanda wa Kaskazini Magharibi kwa kuanzisha utalii wa maji katika Ziwa Victoria na Ghuba ya *Speke*. Jitihada hizo, zitachangia ongezeko la idadi ya watalii, wastani wa muda wa mtalii kukaa nchini na mapato yatokanayo na shughuli za kitalii.

**(v) Kupandishwa Hadhi Maeneo ya Hifadhi**

**17.** ***Mheshimiwa Spika***, katika jitihada za kuhifadhi rasilimali za misitu, Wizara imepandisha hadhi Msitu wa Essmingori uliopo Wilaya ya Monduli wenye hekta 6,070 kuwa Hifadhi ya Msitu ya Mazingira Asilia na hivyo kuongeza hifadhi za misitu ya mazingira asilia kutoka 19 hadi 20. Aidha, Wizara imepandisha hadhi maeneo 30 mapya ya misitu yenye ukubwa wa jumla ya hekta 139,869 kuwa hifadhi. Sambamba na hatua hiyo, hifadhi za nyuki sita (6) zenye ukubwa wa hekta 19,134 zimetangazwa na hivyo kuongeza idadi ya hifadhi za nyuki kutoka moja (1) hadi saba (7).

(vi) Kuongezeka kwa Mashamba na Upandaji Miti

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imeanzisha mashamba mapya mawili (2) ya miti ya Makere Kusini lililopo katika Wilaya ya Kasulu lenye hekta 30,000 na Mwanhala lililopo Wilaya ya Nzega lenye hekta 3,000 na hivyo kuongeza idadi ya mashamba ya miti ya Serikali Kuu kutoka 23 hadi 25. Kwa upande mwingine, Wizara imefanikiwa kuzalisha jumla ya vipando vya mikoko 52,790 na miche ya miti milioni 32.33 iliyopandwa katika mashamba ya Serikali, taasisi za umma na binafsi. Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau wakiwemo wananchi imepandwa jumla ya miche milioni 3.51 katika maeneo tofauti ya Jiji la Dodoma. Jitihada hizi zimelenga kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi na kuhakikisha upatikanaji wa mazao ya misitu kwa matumizi mbalimbali.

(vii) Kuboreshwa na Kuimarika kwa Vituo vya Malikale

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha maeneo ya malikale yanaimarika na kuvutia watalii, Wizara imeboresha vituo vya malikale kwa kujenga barabara yenye urefu kwa kilomita tano (5), ukuta na njia ya watembea kwa miguu katika Kituo cha Kolo; kuweka umeme katika Kituo cha Mapango ya Amboni; na kukarabati jengo la kihistoria la soko la watumwa katika Kituo cha Mikindani. Sambamba na hilo, Wizara imeanza kuhifadhi taarifa za maeneo ya malikale, mikusanyo na urithi wa utamaduni kidijitali, hatua ambayo itasaidia kuimarisha uhifadhi na kujitangaza kidijitali.

(viii) Kupungua kwa Ujangili na Uvunaji Haramu wa Maliasili

20. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kuimarisha ulinzi wa rasilimali za maliasili kwa kudhibiti ujangili, biashara haramu ya nyara na uvunaji haramu wa mazao ya misitu. Mathalan, matokeo ya sensa ya mwaka 2020 yameonesha kuongezeka kwa idadi ya tembo katika Mfumo Ikolojia Serengeti kutoka 6,087 mwaka 2014 hadi 7,061 mwaka 2020. Kwa ujumla mafanikio haya yamechangiwa pamoja na mambo mengine, kuendeshwa kwa siku doria 746,413; kuvunjwa kwa mitandao 95 ya ujangili; na kuzuiliwa kwa matukio 302 ya ujangili kabla hayajatendeka. Kutokana na juhudi hizo, ujangili umepungua kwa takriban asilimia 90.

3.4 UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA SEKTA YA WANYAMAPORI

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Wanyamapori ina jukumu la kuhifadhi, kusimamia, kutoa mafunzo na kufanya tafiti za wanyamapori ndani na nje ya maeneo yaliyohifadhiwa. Katika mwaka wa fedha 2021, Wizara imetekeleza shughuli mbalimali kama ifuatavyo: -

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, Wizara imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utatuzi wa Migogoro baina ya Wanyamapori na Binadamu (2020 - 2024). Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri mbalimbali imeendelea kufanya doria na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu. **Kwa namna ya kipekee naomba nitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa mara ya kwanza Wizara ilizindua namba maalum za simu (hotlines) ambazo siyo za kulipiwa kwa ajili ya kupata taarifa kwa haraka kuhusu matukio hayo.**

23. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, Wizara imekamilisha maandalizi ya Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu; na kuandaa Mtaala wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu utakaotumika kutoa mafunzo kwa watumishi. Aidha, Wizara imefanya mapitio ya Kanuni za uwindaji wa wenyeji; mashamba, bustani na ranchi za wanyamapori; uuzaji wa nyamapori; uwindaji wa kitalii; na maeneo maalum ya uwekezaji kwenye hifadhi za wanyamapori - SWICA. Vilevile, Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara umefanyiwa mapitio kwa ajili ya kuandaa Mkakati mpya.

(i) Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania - TANAPA

24. ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika la Hifadhi za Taifa lina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji utalii kwenye hifadhi za Taifa 22. Katika kutekeleza jukumu hilo, Shirika imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuboresha mahusiano kati ya hifadhi na jamii ambapo elimu ya uhifadhi imetolewa kwa vijiji 402; kuvijengea uwezo vikundi 54 vinavyopakana na hifadhi za Taifa kwa lengo la kuviwezesha kushiriki katika kukabiliana na ujangili; na kuwapatia watumishi 460 mafunzo ya ukarimu kwa wateja. Katika hatua nyingine, Shirika limetenga maeneo mapya 45 ya huduma za malazi yenye uwezo wa vitanda 3,250 kwa ajili ya uwekezaji katika hifadhi za Taifa. Sambamba na hilo, madaraja mawili (2) katika Hifadhi ya Taifa Tarangire na Kitulo yamejengwa, kilometa 7,100 za barabara katika hifadhi za Taifa 18 zimekarabatiwa na kiwanja cha ndege katika Hifadhi ya Taifa Mto Ugalla kimejengwa.

25. ***Mheshimiwa Spika***, Kazi nyingine zilizotekelezwa na Shirika ni pamoja na: kununua boti mbili (2) na injini mbili (2) za boti kwa ajili ya kuimarisha doria katika Hifadhi ya Taifa Nyerere; na kununua magari 35 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za uhifadhi na uendelezaji utalii katika hifadhi za Taifa. Sambamba na hilo, Shirika limefanya jumla ya siku doria 251,926 kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika hifadhi. Jitihada hizi zimewezesha kudhibiti ujangili ndani ya hifadhi za Taifa na hivyo kufanya rasilimali hizo kuendelea kuchangia ipasavyo katika uchumi wa nchi.

(ii) Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania - TAWA

26. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania ina jukumu la kusimamia uhifadhi na kuendeleza utalii katika mapori ya akiba, mapori tengefu na maeneo matatu ya ardhioevu pia ni mwangalizi na mshauri wa shughuli za uhifadhi katika maeneo 38 ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori - WMAs, mashamba, bustani, ranchi na Kituo cha kulelea wanyamapori wenye matatizo mbalimbali. Katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Mamlaka imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kufanya siku doria 99,341; kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kuepuka na kujikinga dhidi ya wanyamapori wakali na waharibifu; na kuanzisha vituo vya Askari vya kudumu kwa ajili ya kuimarisha doria za kudhibiti wanyamapori wakali na waharibifu katika maeneo yenye matatizo hayo.

27. ***Mheshimiwa Spika***, kazi nyingine zilizotekelezwa na Mamlaka ni: kukamilisha ujenzi wa njia za watembea kwa miguu zenye urefu wa mita 850 katika eneo la Hifadhi ya Magofu ya Kilwa Kisiwani (mita 700) na Pori la Akiba Mpanga Kipengere (mita 150); na kuendesha minada kwa njia ya kielektroniki badala ya utaratibu wa awali wa ugawaji vitalu kupitia kamati maalum. Aidha, Mamlaka imeendelea kutumia kikosi cha mbwa wanusao katika viwanja vya ndege vya kimataifa vya Kilimanjaro (KIA) na Julius Nyerere (JNIA) ili kudhibiti usafirishaji haramu wa nyara za Serikali.

(iii) Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro - NCAA

28. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro ina jukumu la kusimamia shughuli za uhifadhi, uendelezaji wa utalii na ustawi wa jamii zinazoishi ndani ya eneo la Hifadhi. Katika kutekeleza jukumu hilo, Mamlaka imefanya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kujenga barabara yenye urefu wa kilometa 4.4 ya kushuka kreta kwa kiwango cha tabaka gumu la mawe na barabara ya kutoka Golini hadi Ndutu yenye urefu wa kilometa 23 ya kiwango cha changarawe; kukarabati barabara zenye jumla ya kilometa 271 ndani ya hifadhi; na kuimarisha nyanda za malisho ndani ya hifadhi kwa kuendelea kutekeleza Mpango Mkakati wa Kutokomeza Mimea Vamizi kwenye eneo la hifadhi. Aidha, kupitia programu ijulikanayo kama Ngorongoro Crater App jina la Hifadhi ya Ngorongoro limepata mwitikio mkubwa kwa kufuatiliwa na watu takriban bilioni 1.8 kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii. Kupitia utaratibu wa masoko mtandao, idadi ya watu duniani wanaofuatilia vivutio vya utalii vilivyopo eneo la Ngorongoro imeongezeka kutoka milioni 1.35 mwezi Juni, 2020 hadi watu milioni 6.96 kufikia mwezi Aprili, 2021. Sambamba na hatua hizo, Mamlaka imeimarisha mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za ujangili, ufuatiliaji wa kila siku wa mtawanyiko wa tembo, faru na wanyama wengine walio hatarini kutoweka kwa kuwawekea vifaa maalum vya kufuatilia mienendo yao.

(iv) Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori - TAWIRI

29. *Mheshimiwa Spika,* Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori ina jukumu la kufanya na kuratibu utafiti wa wanyamapori nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa kipindi cha mwaka 2020/2021 Taasisi hii pamoja na kazi nyingine imeidadi wanyamapori katika Mfumo Ikolojia Serengeti; hifadhi za Taifa Burigi - Chato na Kigosi; na Pori la Akiba Moyowosi. Matokeo ya zoezi hilo yanaonesha kuwa kuna idadi ya tembo 7,061, nyati 69,075 na twiga 6,680 katika Mfumo Ikolojia wa Serengeti; na pundamilia 182, pofu 209 na swala pala 251 katika Hifadhi ya Taifa ya Burigi - Chato. Aidha, Taasisi imeendelea kufuatilia afya za wanyamapori kwa kutoa tiba kwa takriban wanyamapori 36 katika mifumo ikolojia mbalimbali; na kufanya utafiti wa ugonjwa unaoathiri twiga katika hifadhi za Taifa za Tarangire, Serengeti na Ruaha. Taasisi pia imefanya uchunguzi wa sababu ya vifo vya viumbe hai mbalimbali wakiwemo faru na tembo (Eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na Mkomazi), viboko (Mto Koga) na ndege maji na samaki (Ziwa Natron). Matokeo ya awali yanaonesha kuwa wanyamapori wakubwa walikufa kwa kula mazao ambayo yalikuwa yamenyunyiziwa viuatilifu ambavyo ni sumu kwa wanyamapori.

(v) Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - CAWM Mweka

30. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021, Chuo cha Usimamizi wa Wanyamapori - Mweka kimedahili jumla ya wanafunzi 929 katika ngazi mbalimbali. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi ya uhifadhi na uongozaji utalii kwa jumla ya washiriki 480. Vilevile, Chuo kimekamilisha ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 200. Sambamba na hilo, Chuo kimekarabati majengo ya utawala, zahanati, mgahawa, madarasa manne (4), hosteli mbili (2) na barabara za ndani. Katika hatua nyingine, Chuo kimeboresha miundombinu katika eneo la mafunzo kwa vitendo lililopo Kwakuchinja wilayani Babati kwa kuweka umeme katika nyumba tatu (3) za watumishi na kambi ya mafunzo; na kuchimba kisima cha maji na kujenga vyoo vya kisasa. Pia, magari makubwa mawili (2) yamenunuliwa kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo.

(vi) Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi

31. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Taaluma ya Usimamizi wa Wanyamapori Pasiansi ina jukumu la kutoa mafunzo ya uhifadhi wa wanyamapori na himasheria katika ngazi ya Astashahada. Katika kutekeleza jukumu hilo, Taasisi imedahili wanafunzi 343 wa fani za uhifadhi wanyamapori na himasheria, uongozaji watalii na usalama kwa ngazi ya Astashahada. Aidha, Taasisi imeandaa mitaala miwili (2) kuhusu uongozaji wa watalii na usalama katika ngazi ya Astashahada na kuboresha mitaala ya usimamizi wa wanyamapori na himasheria. Pia, Taasisi inaendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maktaba.

(vii) Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu- Sekamaganga

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Kituo cha Mafunzo ya Uhifadhi wa Maliasili kwa Jamii, Likuyu - Sekamaganga kina jukumu la kuzijengea uwezo jamii zinazoishi jirani na maeneo yaliyohifadhiwa kushiriki katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kituo kimeanzisha kozi mpya ya Astashahada ya Awali ya Waongoza Watalii. Aidha, Kituo kimetoa mafunzo ya usimamizi wa rasilimasili za maliasili kwa askari wa wanyamapori 151 wa vijiji katika Maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori pamoja na maeneo ya misitu ya Serikali. Vilevile, Kituo kimejenga bwalo na jiko na kununua vifaa vya mafunzo kwa ajili ya kufundishia.

SEKTA YA MISITU NA NYUKI

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Misitu na Nyuki ina jukumu la kusimamia uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki. Katika kutekeleza jukumu hilo, sekta ya misitu na nyuki imetekeleza shughuli zifuatazo: kuendelea kutoa elimu, kuhamasisha na kuwezesha wadau mbalimbali kuanzisha viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu na nyuki; kuandaa mipango 37 ya uvunaji wa mazao ya misitu katika misitu ya vijiji na matajiwazi; na kununua mashine mbili (2) za kisasa za kuchakata magogo ili kuongeza thamani ya mazao ya misitu; kukarabati njia za asili za watalii zenye urefu wa kilometa 73.3, barabara zenye urefu wa kilometa 128.8 na ujenzi wa maeneo mawili (2) ya kuweka mahema ya muda ya kitalii katika hifadhi za misitu ya mazingira asilia; na kuandaa Kanuni za Uwekezaji wa Utalii kwenye maeneo ya hifadhi ya misitu.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zilizofanyika ni: kufanya tathmini na mapitio ya miongozo ya sera za sekta za misitu na nyuki na kuandaa mikakati ya utekelezaji wake; kuandaa kanuni za Uendeshaji wa Tafiti za misitu kwa Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania za mwaka 2020, Tozo ya Mazao na Huduma za Misitu za mwaka 2020 pamoja na Kanuni za Mfuko wa Misitu za Kusimamia Utoaji wa Ruzuku za mwaka 2021. Vilevile, Wizara imeandaa miongozo minne (4) ya Kusimamia Shughuli za Uendeshaji wa Mashamba ya Miti wa mwaka 2021, Mafunzo na Huduma za Ugani za Ufugaji Nyuki wa mwaka 2020, Uanzishaji na Usimamizi wa Hifadhi za Nyuki na Manzuki wa mwaka 2021, Taratibu za Utoaji Mafunzo na Huduma za Ugani katika Ufugaji Nyuki za mwaka 2021 pamoja na mwongozo wa Matumizi ya Miti ya Misaji na Miti Mingine wa mwaka 2021. Miongozo hii itaimarisha usimamizi na uendelezaji wa sekta ya misitu na nyuki na kuongeza tija pamoja na mapato ya Serikali.

(i) Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania - TFS

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Huduma za Misitu una jukumu la kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu na nyuki katika maeneo ya misitu 463 iliyohifadhiwa kisheria. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wakala umeimarisha shughuli za ukaguzi wa mazao ya misitu na nyuki kwa kufanya siku doria 3,529 katika misitu yote ambayo ipo chini yake. Aidha, Wakala umeandaa mipango mipya ya usimamizi wa misitu 11 yenye jumla ya hekta 243,508. Katika hatua nyingine, Wakala umeendelea kutekeleza na kuwezesha

shughuli za upandaji miti katika mashamba ya Serikali, maeneo ya watu binafsi na taasisi mbalimbali. Katika hatua hiyo, tani 7.78 za mbegu bora za miti zimezalishwa, miche 32,331,910 na vipando 52,790 vya mikoko vimeoteshwa.

**36.** ***Mheshimiwa Spika***, Wakala pia umeimarisha mipaka ya misitu kwa kuhakiki kilometa 97, kusafisha kilometa 1,219, kuweka vigingi 595 na kuweka mabango 180 katika misitu mbalimbali. Sambamba na hilo, Wakala umesafisha njia za kudhibiti moto kwenye misitu ya asili na mashamba ya miti yenye urefu wa kilometa 2,433. Katika hatua nyingine, Wakala umeendelea kuhudumia manzuki 181 ambazo zimeweza kuzalisha tani 12.9 za asali na kilo 601.86 za nta. Aidha, Wakala umeanzisha vikundi vipya 54 vya ufugaji nyuki na kutoa elimu ya ufugaji bora wa nyuki kwa wafugaji 1,751 ili kuwawezesha kujiongezea kipato.

**(ii) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania - TAFORI**

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania ina jukumu la kufanya na kuratibu utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu wa misitu na ufugaji nyuki nchini. Katika kutekeleza majukumu yake, Taasisi imefanya utafiti ili kubaini ubora na thamani halisi ya spishi saba (7) za miti ya mbao. Utafiti huo ulihusisha spishi za miti ya mkuruti, mgonga chuma, mgama, mbebeti, mnangu mweusi, mtunda na mnake mweusi. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa mbao za miti hiyo zina viwango vya ubora kwa matumizi ya ujenzi wa madaraja, nyumba, boti na kutengeneza samani. Miti hii itapunguza utegemezi wa matumizi ya mbao zilizozoeleka za miti ya mninga na mkongo na kuongeza mchango wa sekta ya misitu katika Pato la Taifa. Aidha, Taasisi imefanya utafiti wa miti inayotumika kama dawa na iliyo hatarini kutoweka kwa lengo la kuitambua na kuihifadhi. Kufuatia utafiti huo, miti ya aina ya nengonengo, mlungulungu na mzima imebainika kutumiwa na wenyeji kama dawa asilia kwa magonjwa mbalimbali ya binadamu.

**(iii) Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Chuo cha Misitu Olmotonyi kimedahili wanafunzi 867 na kuboresha miundombinu kwa kuendelea na ujenzi wa jengo la utawala. Chuo cha Viwanda vya Misitu kimedahili wanafunzi 224 na kimekarabati madarasa matatu (3), geti moja (1) na kujenga kingo za barabara za ndani ya Chuo. Aidha, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimedahili wanafunzi 408 na kinaendelea kuboresha miundombinu kwa kujenga jengo la kiwanda cha kuchakata mazao ya nyuki pamoja na ukarabati wa jengo la utawala.

**SEKTA YA UTALII**

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Utalii ina jukumu la kusimamia, kuendeleza na kutangaza utalii nchini. Katika kutekeleza jukumu hilo, Wizara imetekeleza shughuli mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati nchini ambayo ni utalii wa mikutano na matukio, fukwe, meli, michezo na utamaduni; kuainisha maeneo ya fukwe yanayofaa kwa ajili ya shughuli za utalii; na kuandaa Mwongozo wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Utalii wa Meli katika Bandari ya Dar es Salaam. Pamoja na jitihada hizo, Wizara pia imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza na kukuza utalii kupitia matukio ya michezo na utamaduni. Kwa ujumla, matukio hayo yamekuwa yakitoa fursa ya kutangaza vivutio vya utalii katika maeneo ya malikale, wanyamapori, misitu na nyuki na hivyo kuwa chachu ya kuhamasisha makundi mbalimbali ya kijamii kushiriki katika utalii wa ndani. Juhudi hizo zitaongeza la idadi ya watalii na ukusanyaji mapato na hivyo kuongeza mchango wa sekta ya utalii katika kukuza uchumi.

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuhamasisha utalii wa ndani, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuanzisha na kuendesha programu na kampeni mbalimbali. Kupitia kampeni hizo, wananchi wamehamasika kutembelea hifadhi, maeneo ya malikale na makumbusho. Kwa upande mwingine, Wizara imeendelea kuendesha mashindano mbalimbali yanayolenga kuibua vipaji na uhamasishaji utalii wa ndani, hususan kwa wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu nchini. Sambamba na hilo, Wizara imeendelea kuimarisha huduma za malazi za bei nafuu katika maeneo yaliyohifadhiwa kwa ajili ya kuchochea utalii wa ndani. Katika hatua nyingine, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imebaini vivutio 51 vya utalii vilivyopo katika mikoa ya Geita, Kagera na Mwanza. Sambamba na hilo, Wizara imehakiki na kuhuisha orodha ya huduma za malazi zinazopaswa kulipa Tozo ya Kitanda Siku. Kazi hii imefanyika katika mikoa 19 na kuwezesha ongezeko la huduma za malazi kutoka 1,238 mwaka 2015 hadi 1,815 mwaka 2020.

**(i) Bodi ya Utalii Tanzania - TTB**

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Bodi ya Utalii Tanzania ilitekeleza shughuli mbalimbali ambazo ni pamoja na: kuandaa na kuzisambaza video mbalimbali za kutangaza utalii kupitia mitandao ya kijamii ambapo jumla ya watu 8,791,000 walifuatilia; kufanya vikao katika kanda sita (6) za kimkakati na Balozi 36 za Tanzania katika nchi mbalimbali duniani kwa njia ya mtandao kwa lengo la kueleza utayari wa Tanzania katika kupokea wageni wakati wa mlipuko wa ugonjwa COVID -19. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na balozi hizo imefanya vikao na wakala wa utalii katika nchi 11. Kutokana na juhudi hizo, nchi imeendelea kupokea makundi ya watalii kutoka nchi mbalimbali duniani.

**(ii) Chuo cha Taifa cha Utalii - NCT**

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Chuo cha Taifa cha Utalii kimedahili jumla ya wanafunzi 1,087 katika ngazi ya Astashahada na Stashahada. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau katika mnyororo wa utalii wapatao 220. Kwa upande mwingine, Chuo kimeanzisha Kampasi mpya ya Mwanza yenye uwezo wa kudahili wanafunzi 550. Sambamba na hilo, Chuo kimefanya mapitio ya mitaala tisa (9) na kuandaa mitaala mipya minne (4) katika fani ya Ukarimu na Utalii. Katika hatua nyingine, Chuo kimefadhili wasichana 35 kushiriki mafunzo ya utalii ngazi ya Astashahada katika Kampasi ya Mwanza.

**SEKTA YA MAMBO YA KALE**

**43.** ***Mheshimiwa Spika***, Sekta ya Mambo ya Kale ina jukumu la kusimamia uhifadhi na uendelezaji wa malikale. Katika kutekeleza jukumu hilo, kwa mwaka 2020/2021, Wizara imebainisha fursa za uwekezaji katika maeneo 18 ya malikale na vituo vya Makumbusho katika mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma, Mara na Arusha. Shughuli za uwekezaji zitakazofanyika katika maeneo hayo ni pamoja na migahawa ya kisasa, studio, maduka ya zawadi, bustani, huduma za kifedha, maduka ya bidhaa za asili na utamaduni na maeneo ya kuweka kambi za utalii za muda. Kutokana na fursa hizo, wadau mbalimbali wanakaribishwa kuwekeza katika maeneo yaliyobainishwa. Vilevile, Wizara imeanzisha mfumo wa kidijitali wa kuhifadhi mikusanyo ya malikale na urithi wa utamaduni katika Makumbusho ya Taifa. Mfumo huu utasaidia kuonesha na kuhifadhi uhalisia wa mikusanyo na maeneo ya malikale kwa muda mrefu. Lengo la Serikali ni kuhakikisha kuwa taarifa za malikale na urithi wa utamaduni zilizopo zinahifadhiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na vijavyo.

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini katika vituo vya malikale vya Kalenga, Isimila, Kunduchi, Bagamoyo na Kilwa Kisiwani. Kufuatia tathmini hiyo, uhakiki wa mipaka umefanyika katika eneo la magofu ya Enguruka wilayani Monduli na kituo cha Zana za Mawe cha Isimila - Iringa ili kuwezesha maeneo hayo kupata hati miliki. Aidha, upimaji wa mipaka umefanyika katika Kituo cha Kalenga, Iringa na Hati ya umiliki kutolewa. Kwa upande mwingine, Wizara imebainisha na kuandaa taarifa za maeneo 34 ya malikale katika mikoa ya Dar es Salaam, Ruvuma na Lindi ili kuhuisha rejesta ya maeneo ya malikale. Sambamba na hilo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeratibu matamasha ya Kumbukizi la Vita vya Majimaji, Kuenzi Azimio la Arusha na Siku ya Kimondo Duniani ambapo elimu ya uhifadhi na uendelezaji wa malikale na urithi wa utamaduni ilitolewa.

**(i) Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania - NMT**

**45.** ***Mheshimiwa Spika***, katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Shirika la Makumbusho ya Taifa limeandaa mpango wa jumla wa uhifadhi na uendelezaji wa maeneo 90 ya malikale. Aidha, ukarabati wa jengo la Soko la Watumwa katika Mji Mkongwe Mikindani umefanyika na kanzidata ya taarifa za mikusanyo ya mji huo imeandaliwa. Pamoja na hatua hiyo, Shirika limeboresha miundombinu ya vituo kwa kukarabati nyumba za asili za baadhi ya makabila kwa kufuata ramani ya Tanzania katika Kituo cha Kijiji cha Makumbusho. Katika hatua nyingine, Shirika limeandaa onesho la historia ya Tanzania kabla ya ukoloni, wakati wa ukoloni na wakati wa harakati za kudai uhuru wa Tanzania. Vilevile, katika kutambua mchango wa wanawake katika harakati za ukombozi wa nchi za Kusini mwa Bara la Afrika, Shirika limeboresha onesho hilo kwa kujumuisha historia ya wanawake walioshiriki katika harakati za ukombozi.

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Shirika limeendelea na zoezi la kukusanya taarifa za kihistoria za Marais kwa ajili ya kutumika kama kumbukumbu kwenye Makumbusho ya Marais itakayojengwa Jijini Dodoma. Aidha, Shirika limeanza maandalizi ya programu ya kuenzi historia na falsafa ya Baba wa Taifa, Mwl. Julius Kambarage Nyerere inayofahamika kama Mwl. Nyerere@100. Sambamba na hatua hiyo, Wizara kupitia Makumbusho ya Taifa imeanzisha klabu za historia na uzalendo mashuleni. Katika kuhakikisha somo la historia na uzalendo linawafikia wanafunzi ipasavyo mashuleni, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imefanikiwa kufungua klabu 16 za historia na uzalendo katika mikoa ya Ruvuma na Dar es Salaam.

**3.5 MIRADI YA MAENDELEO**

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2020/2021 Wizara imeendelea kutekeleza miradi sita (6) ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Nyanda za Juu Kusini - REGROW; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili; Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; na Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu – FORVAC.

**48.** ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 yamefafanuliwa kuanzia **ukurasa wa 9 hadi ukurasa wa 102 katika Kitabu cha Hotuba.**

**3.6 CHANGAMOTO NA UTATUZI**

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imekabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na: mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 duniani ambao kwa kiasi kikubwa umeathiri sekta ya utalii na hivyo kupungua kwa mapato yanayotokana na sekta hiyo; kuwepo kwa mimea vamizi katika baadhi ya maeneo ya hifadhi, hali iliyosababisha kuathirika kwa uoto wa asili na kupungua kwa malisho ya wanyamapori; uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa kwa shughuli za kibinadamu; uwepo wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori; mlipuko wa magonjwa kati ya binadamu na wanyamapori; na uwepo wa matukio ya moto katika maeneo ya hifadhi.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha mwaka 2020/2021, Wizara imeandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Shughuli za Sekta ya Utalii katika kipindi cha COVID-19; na kuandaa Mpango wa Kuirejesha Sekta ya Utalii Nchini katika Hali ya Awali kabla ya Kuathiriwa na COVID-19. Aidha, Wizara imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukabiliana na mimea vamizi ndani ya maeneo ya hifadhi kwa kufanya tafiti na kutekeleza Mpango Mkakati wa Kutokomeza Mimea Vamizi. Vilevile, Wizara imeendelea kuimarisha mipaka ya maeneo hayo, kushirikisha jamii katika uhifadhi, kuwawezesha wananchi kuanzisha miradi ya kijamii na ya ujirani mwema na kutoa elimu kwa jamii kuhusu umuhimu wa maeneo ya hifadhi za maliasili na malikale.

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na uwepo wa migogoro kati ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu kwa wananchi na mali zao, Wizara imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha udhibiti wa wanyamapori husika. Mikakati hiyo ni pamoja na kuimarisha vikosi vya kudhibiti wanyamapori hao, kutumia mbinu za kielektroniki za kufuatilia mienendo ya makundi ya wanyamapori kwa kuwafunga vifaa maalum hasa katika maeneo yenye matukio mengi pamoja na kutoa elimu ya namna ya kujikinga. Katika hatua nyingine, Wizara imezindua namba maalum za simu (hotlines) kwa ajili ya kupata taarifa kwa haraka kuhusu matukio hayo. Sambamba na hatua hizo, Wizara imeandaa mipango ya usimamizi na udhibiti wa moto na kuendelea kutoa elimu kwa jamii zinazopakana na maeneo yaliyohifadhiwa.

**MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2021/2022 kwa kuzingatia miongozo mbalimbali ikiwemo Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya 2020 – 2025. Maeneo ya mpango huo ni Pamoja na:-

**3.7 UKUSANYAJI MADUHULI**

**53.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa mwaka wa fedha 2021/2022, makadirio ya maduhuli yatakayokusanywa na Sekta ya Maliasili na Utalii ni jumla ya **Shilingi bilioni 689.34**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 478.01** zitakusanywa kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana na vyanzo vya TANAPA, NCAA na TAWA na **Shilingi bilioni 211.33** zitakusanywa kupitia Wizara na Taasisi zake. Utaratibu wa ukusanyaji wa mapato umezingatia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2020 ambapo mapato yanayotokana na rasilimali za maliasili na utalii yanakusanywa na Wizara ya Maliasili na Utalii pamoja na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia TRA.

**3.8 MATUMIZI YA KAWAIDA NA MAENDELEO**

**54.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022, Wizara na Taasisi zake inakadiria kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 571.63.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 418.86** ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na **Shilingi bilioni 152.77** za Miradi ya Maendeleo. Aidha, naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kwamba**,** Bajeti ya Wizara mwaka 2021/2022 imeongezeka kwa **Shilingi bilioni 457.04** sawa na ongezeko la **asilimia 399** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2020/2021 ambayo ilikuwa **Shilingi bilioni 114.59.** Ongezeko hili pamoja na

mambo mengine limetokana na kujumuishwa kwa bajeti za TANAPA, NCAA na TAWA katika Bajeti Kuu ya Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii.

**3.9 KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA NA WIZARA NA TAASISI ZAKE**

**SEKTA YA WANYAMAPORI**

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022, Wizara itatekeleza mipango mbalimbali ikiwa ni pamoja na: kuandaa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa kuhifadhi Wanyamapori (2021/2022- 2031/2032); kukamilisha uandaaji wa Mpango Mkakati wa Kitaifa wa Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara (2021/2022 - 2031/2032); kuendelea kudhibiti matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu; kuratibu utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo ya hifadhi; kuboresha usimamizi wa shoroba za wanyamapori na kufanya tathmini ya hali ya mapori tengefu ili kupunguza migongano baina ya binadamu na wanyamapori. Aidha, Wizara itachimba visima nane (8) katika hifadhi za Taifa za Ruaha na Katavi na kufanya ukarabati wa mabwawa matano (5) yenye jumla ya mita za ujazo 98,065 katika hifadhi za Taifa Serengeti, Mkomazi na Saadani kwa ajili ya upatikanaji wa maji kwa wanyamapori wakati wa kiangazi; kupanua wigo wa uwekezaji kwenye hifadhi za Taifa kwa kutenga maeneo 103 ya ujenzi wa loji na kambi za kudumu kwa ajili ya malazi ya wageni yenye uwezo wa vitanda 4,604 katika hifadhi za Taifa mbalimbali zikiwemo Mkomazi, Kitulo, Nyerere, Ruaha, Ibanda – Kyerwa na Rumanyika – Karagwe.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na shughuli hizo, Wizara itaendelea kuboresha huduma za utalii zikiwemo ujenzi wa barabara mpya zenye urefu wa kilometa 2,532 katika Hifadhi ya Taifa na eneo la Hifadhi ya Ngorongoro na kukarabati njia za watalii kutembea kwa miguu zenye urefu wa kilometa 841; kujenga viwanja vipya vya ndege 14 katika hifadhi za Taifa Ruaha, Mikumi na Nyerere na vituo vya utalii vitano (5) katika hifadhi za Taifa Serengeti, Ruaha, Mikumi, Milima ya Udzungwa na Nyerere. Kwa upande mwingine, Wizara itapandisha hadhi msitu wa hifadhi wa Matogoro kuwa hifadhi ya mazingira asilia. Hatua hii inatokana na umuhimu wa ikolojia na bioanuai zilizopo ndani ya hifadhi ya msitu huo na uwepo wa milima ya Matogoro yenye miamba iliyofanyiwa tafiti kwa ajili ya utalii jiolojia *(Geopark).*

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Ibara ya 67(a)(i) ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya 2020 - 2025 inayoelekeza Wizara ya Maliasili na Utalii kukuza na kuimarisha utalii wa uwindaji wa wanyamapori, Wizara imebuni mkakati unaovutia mitaji mikubwa na kwa muda mrefu katika maeneo maalum ya vitalu vya uwindaji ujulikanao kama ***Special Wildlife Investment Concession Area (SWICA).*** Katika kutekeleza mkakati huo, Wizara imetunga kanuni za kuongoza uwekezaji huo ***(The Wildlife Conservation - Special Wildlife Investment Concession Areas) Regulations, 2021).*** Pamoja na masuala mengine, kanuni hizo zinatoa utaratibu wa uwekezaji unaolenga kuimarisha Uhifadhi wanyamapori, kuendeleza biashara ya utalii na kuboresha huduma za utalii nchini kwa kushirikisha jamii. Kwa kutekeleza mpango huo, mapato yanayotokana na uwindaji wa kitalii yataongezeka takriban mara tatu ya uwezo wa sasa wa uzalishaji wa vitalu hivyo na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania. Hii ni kutokana na upembuzi yakinifu wa modeli ya kifedha (**financial model**) iliyofanyika. Aidha, shughuli nyingine zitakazofanyika zinazojumuisha utafiti, mafunzo na uendelezaji wa uhifadhi kwa ujumla zitatekelezwa na Wizara kupitia TAWIRI, Chuo cha MWEKA, Taasisi ya Pasiansi na Chuo cha Likuyu Sekamaganga.

**SEKTA YA MISITU NA NYUKI**

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha sekta ya misitu na nyuki, Wizara itafanya mapitio ya Sheria ya Misitu na Ufugaji Nyuki za Mwaka 2002 na itatafsiri Sheria, Kanuni na Miongozo ya Idara kwa lugha ya Kiswahili; kuandaa mikakati ya Kitaifa ya uendelezaji uongoaji wa ardhi, uwekezaji kwenye biashara ya mazao ya nyuki pamoja na Mpango wa Utekelezaji wa Usimamizi Shirikishi wa Misitu ya Jamii; kuandaa mwongozo wa usimamizi wa mashamba ya miti pamoja na rejesta ya wafugaji nyuki. Aidha, Wizara itaendelea kuratibu siku ya upandaji miti Kitaifa, siku ya misitu duniani na siku ya nyuki duniani; na kuwezesha utoaji wa mafunzo kwa vyama vya ushirika na wadau wengine wa ufugaji nyuki.

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuhudumia mashamba 23 ya miti yenye ukubwa wa hekta 445,354.7 kwa kuzalisha tani 22 za mbegu bora za miti; kuotesha miche 33,185,000; kupanda miti kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 7,833; kupalilia hekta 44,430; kupogoa miti hekta 13,773; kuanzisha mashamba mawili mapya ya miti yenye ukubwa wa hekta 84,500 pamoja na kukamilisha taratibu za kuhifadhi kisheria maeneo mapya yenye ukubwa wa hekta 121,100. Kwa upande mwingine, Wizara itashirikiana na Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi katika vijiji 40. Vilevile, mipaka ya misitu 183 itaimairishwa kwa kupima upya na kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilometa 314.84, kusafisha mipaka yenye kilomita 2,592.28, kuweka vigingi 1,452 na mabango 1,958. Aidha, katika kuimarisha ulinzi na kudhibiti uharibifu wa misitu, Wizara itaandaa mipango ya usimamizi wa misitu 58 yenye ukubwa wa hekta Milioni 1.27. Pamoja na hatua hizo, TFS itaendelea kuchangia shughuli za maendeleo ya jamii kwa kutoa vifaa vya ujenzi katika Serikali za vijiji vitano (5), shule 578 na taasisi 206.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2021/2022, TFS itatoa mafunzo ya usimamizi wa misitu kwa Kamati za Maliasili za Vijiji 97 kwa ajili ya kuziongezea uwezo wa kulinda na kusimamia rasilimali za misitu. Aidha, wananchi na wadau wengine wa mazingira watashirikishwa kupanda miti 7,070,000 katika maeneo mbalimbali ikiwemo mashambani, maeneo yaliyoharibika pamoja na kandokando ya vyanzo vya maji. Kati ya miche hiyo, miche 1,000,000 itapandwa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma katika kuendeleza kampeni ya *Dodoma ya Kijani*. Vilevile, TFS Itaendelea kuimarisha rasilimali za nyuki kwa kusimamia manzuki 181 za nyuki na kuzalisha tani 96 za asali na tani saba (7) za nta Pamoja na kuanzisha mashamba matatu (3) maalum ya nyuki katika wilaya za Kondoa, Songea na Manyoni. Pia, Wakala utapandisha hadhi maeneo yenye ukubwa wa hekta 630.8 kuwa hifadhi za nyuki. Kwa upande mwingine, Wakala utatoa mafunzo ya mbinu bora za ufugaji nyuki kwa taasisi 20, vikundi 138 vyenye wafugaji 1,490 na kutoa mizinga 1,000 na seti 100 za mavazi.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika kuchangia uendelezaji wa viwanda nchini, Wakala utaendelea kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vya misitu ambapo unatarajiwa kuuza mita za ujazo 1,082,903 kutoka mashamba ya miti 13 na zaidi ya mita za ujazo 700,000 kutoka misitu ya asili. Aidha, katika kuongeza ufanisi wa sekta ya misitu na nyuki shughuli za utafiti, utoaji mafunzo, uendelezaji wa mazao ya misitu na nyuki na uwezeshaji zitaendelea kutekelezwa na Wizara kupitia Taasisi ya TAFORI, Chuo cha Viwanda vya Misitu, Chuo cha Misitu Olmotonyi na Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora na Mfuko wa Misitu Tanzania.

**SEKTA YA UTALII**

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara itaendelea kufanya mapitio ya Sheria ya Utalii Sura 365 na Kanuni zake pamoja na kukamilisha Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999. Kwa upande mwingine, Wizara itaendelea na jitihada za kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo utalii wa fukwe, utalii wa meli pamoja na kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Utalii wa Mikutano na Matukio. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kuchukua hatua za kuirejesha sekta ya utalii katika hali yake ya awali baada ya athari za COVID-19. Hatua hizo ni pamoja na kuendelea kutekeleza Mpango wa Kurejesha Sekta ya Utalii katika Hali ya Awali (2020/2021 - 2024/2025) baada ya mlipuko wa janga la COVID-19. Sambamba na hatua hizo, Wizara itaimarisha mfumo wa kielektroniki wa kupanga huduma za malazi nchini katika daraja za ubora – AserT pamoja na kutoa mafunzo kwa watoa huduma za malazi katika mikoa 12 kuhusu mfumo huo.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuimarisha ushiriki wa wadau katika kuendeleza sekta ya utalii nchini kupitia jukwaa la majadiliano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi pamoja na mikutano ya Kamati ya Uwezeshaji wa Masuala ya Utalii. Aidha, Wizara kupitia TTB itatumia mbinu mbalimbali kutangaza utalii ndani na nje ya nchi kwa kuratibu na kushiriki maonesho ya utalii katika masoko ya msingi, kimkakati na yale yanayoibukia yakiwemo Marekani, Urusi, China, India, Australia, Israel, nchi za Bara la Ulaya, Falme za Kiarabu na Kanda ya Afrika. Vilevile, itaimairisha ushirikiano na Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi na kuanza utaratibu wa kuzishindanisha kwa kutoa motisha ili ziendelee kutangaza utalii kwa ufanisi zaidi. Katika hatua nyingine, Wizara itaendelea kutangaza utalii kupitia maonesho na matamasha mbalimbali yakiwemo: Karibu - Kili Fair, Siku ya Utalii Duniani na Karibu Kusini; matamasha ya Majimaji na Siku ya Vimondo Duniani; Rock city Marathon, Kili Marathon na Mbeya Tulia Marathon, Majimaji Selebuka Festival, East Africa Trade Fair na Lamadi Utalii Festival.

**64.** ***Mheshimiwa Spika***, kwa namna ya kipekee naomba nilitaarifu Bunge lako Tukufu Serikali kupitia **Wizara itaanzisha utalii mahsusi wa lugha ya kiswahili (Swahili Tourism Package)**. **Katika aina hii ya utalii, mtalii ataunganishiwa vifurushi mbalimbali vya utalii ambavyo vinaendana na lugha husika**. Mathalan, mtalii ataweza kulipa mara moja na kuwezeshwa kupata muda wa kujifunza lugha ya kiswahili kwa hatua ya awali; kununua bidhaa za Kitanzania (mfano vitenge, khanga na vinyago); na kuandaliwa matukio mbalimbali ya kiutamaduni yakiwemo ngoma na vyakula vya asili. Aidha, Wizara kupitia Chuo cha Taifa cha Utalii itaendelea kutoa mafunzo katika fani za ukarimu na utalii kwa lengo la kuboresha huduma za utalii nchini.

**SEKTA YA MAMBO YA KALE**

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika sekta ya mambo ya kale, Wizara itatekeleza masuala mbalimbali yakiwemo: kufanya mapitio ya Sheria ya Mambo ya Kale Sura 333 na Sheria ya Makumbusho ya Taifa Sura 281; kuandaa miongozo ya uhifadhi wa malikale, utafiti na uwekezaji; kuandaa mkakati wa utekelezaji wa Sera ya malikale; na kuhakiki na kupima mipaka ya maeneo 15 ya malikale. Aidha, Wizara kupitia Shirika la Makumbusho ya Taifa itatekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo: ujenzi wa Makumbusho ya Marais itakayojengwa Jijini Dodoma; kuweka onesho la Kudumu la Tembo katika Makumbusho ya Elimu Viumbe Arusha; kuendelea kushirikisha wadau katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maeneo ya malikale; na kuendelea kutangaza vivutio vya malikale na makumbusho. Aidha, Shirika litaendeleza programu mbalimbali za kutoa elimu ya historia na uzalendo nchini kwa kufungua klabu 220 katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Dodoma na Singida.

**MIRADI YA MAENDELEO**

**66.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2021/2022 Wizara itatekeleza miradi nane (8) ya maendeleo ambayo ni: Mradi wa Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Ukanda wa Kusini (REGROW); Mradi wa Kujenga Uwezo wa Maeneo ya Hifadhi, Mapori ya Akiba na Kikosi Dhidi ya Ujangili; Mradi wa Kuzuia na Kupambana na Ujangili na Biashara Haramu ya Nyara; Mradi wa Panda Miti Kibiashara; Mradi wa Kujenga Uwezo wa Taasisi za Mafunzo ya Misitu na Ufugaji Nyuki; Mradi wa Kuongeza Thamani kwa Mazao ya Misitu (FORVAC); Mradi wa Uendelezaji wa Utalii wa Mikutano na Matukio (MICE); na Mradi wa Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki (BEVAC).

**67.** ***Mheshimiwa Spika***, maelezo ya kina kuhusu shughuli na miradi itakayotekelezwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/2022 yamefafanuliwa kuanzia **ukurasa 106 hadi ukurasa 152 katika Kitabu cha Hotuba.**

**4.0 SHUKRANI**

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kutumia nafasi hii tena kuwashukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge kwa ushirikiano mnaotoa katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Pia, ninawashukuru wadau wote kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Kipekee, nizishukuru nchi marafiki, washirika wa maendeleo, mashirika ya kimataifa, taasisi za kiserikali pamoja na wadau wengine wakiwemo sekta binafsi. Nachukua fursa hii kutaja baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali za Canada, China, Korea Kusini, Marekani, Norway, Ubelgiji, Ufini, Ujerumani, Uswisi na Jumuiya ya Umoja wa Nchi za Ulaya. Mashirika na taasisi za Kimataifa ni pamoja na: AfDB, AWF, AWHF, FAO, FZS, GEF, GIZ, ICCROM, ICOM, ICOMOS, ILO, IUCN, KfW, NORAD, PAMS Foundation, Trade Aid, UNDP, UNESCO, UNWTO, USAID, WCS, WHC, WTTC, World Bank, Wild Aid, WMF na WWF. Aidha, ninapenda kuwashukuru wananchi wote walioshiriki kikamilifu katika shughuli za uhifadhi wa maliasili, malikale na uendelezaji utalii. Ninatoa rai kwa wadau wote kuendelea kutoa ushirikiano wa dhati kwa Wizara ili iweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Ni matumaini yangu kuwa kupitia ushirikiano huu malengo ya uhifadhi yatafikiwa kwa haraka na kwa ufanisi zaidi.

**5.0 MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2021/2022**

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya **Shilingi 571,632,424,000** kwa matumizi ya **Fungu 69** - Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha 2021/2022. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 418,859,544,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 152,772,880,000** ni za miradi ya maendeleo.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** fedha za matumizi ya kawaida zinajumuisha **Shilingi 153,537,684,000** za mishahara na **Shilingi 265,321,860,000** za matumizi mengineyo. Aidha, fedha za miradi ya maendeleo zinajumuisha **Shilingi 113,893,184,000** fedha za ndani na **Shilingi 38,879,696,000** fedha za nje.

**6.0 HITIMISHO**

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuhitimisha kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako wewe na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maliasili na Utalii: **www.maliasili.go.tz**

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

## SIKU YA HEDHI

# 'Wenye jambo lao' wapigana kutafuta haki iliko, shinikizo iwamo katika bajeti

## ■Meya, Diwani watikisa kichwa 'ndio'

Na Yasmine Protace

INAWEZEKANA kudiriki kutamka hedhi salama sasa ni kampeni rasmi kitaifa, katika sura tofauti. Sura ya utetezi ikitoka pande nyingi za umma, ngome kuu ni kutoka kwa kinamama.

Muhimu katika hilo ni nini? Inatakiwa mtu azingatie, tena iwe kwa msichana au mwanamke, katika kuepuka maambukizi ya magonjwa.

Pamoja na kudai hedhi salama kwa wanawake na watoto shule, pia kumekuwapo shida kubwa kwa baadhi ya familia zinazoshindwa kumudu gharama za taulo za kike.

Uhalisia uliopo, ni kwamba hadi sasa kuna familia ambazo zina wakati mgumu kumudu namna ya kusimamia maisha yao kila siku, hata kuthubutu milo milo mitatu.

Hiyo, pia iko katika sura nyingine, mtihani mgumu katika harakati za kumudu kununua taulo za kike kwa mabinti au kinamama na haishangazi kuiwashuhudia mabinti na hasa shuleni, wanajistiri kwa vifaa visivyofaa.

### KUTOKA MAADHIMISHO

Katika kusherehekea maadhimisho ya Siku ya Hedhi Duniani ,baadhi ya washiriki waliomba taulo za kike ziwe zinatolewa bure kama ziavyogaiwa mipira ya kiume, maarufu kondomu.

Bishagazi Delema, ni Mwenyekiti wa Kituo cha Maarifa na Taarifa, kilichopo Kipunguni jijini Dar es Salaam, anasema kuwa serikali inapaswa kufanya mpango wa kutoa bure taulo za kike kwa mabiniti, kama kondomu zinavyotokewa bure katika baadhi ya maeneo.

Anasema, katika baadhi ya ofisi kondomu zinawekwa mpaka vyooni kuhamamsisha kinga, katika kusherehekea baadhi ya maadhimisho, kila atakaye inakuwa ruksa kwake kuchukukua.

"Tukumbuke kuwa kuna watu waishio maisha magumu, hata milo mitatu kwa siku hawapaki, sasa watawezaje kumudu kununua taulo za kike," anahoji.

Anaongeza kuwa wananchi wanapaswa kujenga utamaduni wa kushiriki mikutano ya kijiji, ili waweze kuizungumzia bajeti yenye mlengo wa kijinsia, itakayokuwa mkombozi kwa mwanamke.

### KIONGOZI MTANDAO

Mwenyekiti wa Mtandao wa Vituo vya Maarifa na Taarifa Ubungo, Neema Mwinyi, anasema vituo vya taarifa na maarifa mkoa Dar es Salaam, vinavyofadhiliwa na asasi TGNP Mtandao, mtazamo wake ni kumkomboa msichana katika bajeti ya mlengo wa kijinsia.

Anasema shule nyingi zinakabiliwa na ukosefu wa maji ndani ya vyoo, ukosefu wa shimo la kuchoma taulo zilizotumika na ukosefu wa vyumba vya kujistiri.

Neema anasema Siku ya Hedhi ina manaa kwa mataifa kujenga uelewa na kupaza sauti katika jinsi ya kupata huduma nzuri za kusaidia wanawake kuwa salama, wanapokuwa kwenye hali hiyo.

Anasema ni ukweli ulio wazi kwamba hata matatizo mengi ya wanawake kuhusiana na uzazi, chimbuko lake ni kushindwa kwao kukabiliana na hedhi kwa njia salama, hasa wanapokuwa katika umri mdogo.

"Umoja wa Mataifa ulilipa uzito wa kipekee siku hiyo, baada ya kuona kwamba kwa nchi zinazoendelea, mwanamke akiwa katika hedhi anapata tabu zaidi kwa sababu vifaa vya kujistiri vina gharama kubwa sana na gharama za kuzimudu hawawezi," anasema.

Pia, anafafanua kwamba wanapokuwa katika maadhimisho hayo, wao kama wadau huwa na utetezi katika usawa wa kijinsia na haki za wanawake wametoa ushauri wao.

Neema anashauri kwamba, jamii zivunje ukimya walio nao kwenye masuala yanayohusiana na hedhi salama na

familia zinapaswa kutoa kipaumbele, katika bajeti inatimiza yaliyo muhimu katika kuhakikisha nyumbani kunapatikana vifaa na nyenzo za kutisha.

Msisitizo wa mama huyo ni kwamba, mara zote hedhi ambayo kibaiolojia ni sehemu ya maisha ya mwanamke na kutokana na uhalisia huo, ni muhimu shule kuwa na mwalimu mlezi anayewasimia mabinti kuwapa ushauri.

Neema anaenda mbali kwamba, halmashauri zinapaswa kutenga bajeti ya kutosha ya kutoa pedi bure kwa mabinti shuleni, sambamba na kuboresha matundu ya vyoo.

### VIONGOZI HALMASHAURI

Hoja ya Neema, inaungwa mkono na Diwani wa Viti Maalumu katika Manispaa ya Ubungo, Dar es Salaam, Kiberatha Samboni, anayesema hedhi salama ni jambo la lazima kwa kila mwanamke na msichana.

Anasema, katika halmasahuri wako katika hatua ya kuamua na itafika wakati watakaoamua, hata kuwa katikia nafasi nzuri ya kulizungumzia suala hilo, shinikinzo lililopo ni katika mwaka ujao wa fedha kutengwe bajeti mahsusi.

Mama huyo diwani, anasema wanatamani taulo za kike zitolewe bure, nao kinamama kwa umoja wao watajitahidi kushawishi zifutiwe kodi, ili raulo hizo ziuzwe kwa bei nafuu.




Waziri Dk. Dorothy Gwajima; wizara yake ni muwajibikaji mkuu katika kutetea hedhi salama. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema tatizo lililopo sasa ni kwamba taulo hizo za kinamama umuhimu wake bado hauchukuliwi kwa mapana, ikiwamo ngazi ya familia kutokana na baadhi ya wazazi hawaoni umuhimu mtoto wa kike kwenda shule pale anapokuwa katika hedhi.

Mtazamo wake ni kuwapo elimu kwa jamii itolewe ili umma uamke na kutambua kwamba kuna umuhimu wanafunzi wa jinsia zote wasaidiane kwa yale yanayolazimika.

Naibu Meya wa Manispaa ya Ubungo, Hassan Siraji, anawataka walimu wa shule za msingi na sekondari nchini kutenga maeneo maalumu kwa ajili ya kuwasaidia watoto wa kike kujistiri, pale wanapokuwa kwenye hedhi.

Anaeleza kuzifahamu baadhi ya shule zenye changamoto ya matundu ya vyoo na maji, akiwa na ufafanuzi:" Hizo changamoto tutazimaliza kupitia fedha za bajeti zilizojengwa kwa ajili ya kutatua kero kwa watoto wa kike."

Naibu Meya anawataka walimu kuwapatia elimu ya hedhi watoto wa Jinsia zote ili waweze kujitambua.

### MWANAFUNZI JE?

Mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Misigani (jina tunalo), anasema kila shule inatakiwa kuwapo na eneo mahususi kwa ajili ya kuchoma taulo za kike pale wanapozibakisha.

Pia, anaongeza haja ya baadhi ya shule zinapasa kuwa maji nje ya vyoo vyao, hilo likiwa ni changamoto pale mtu anapotaka kujisitiri, huwa anaangukia magumu.

Hoja yake anaianua kuwapo haja ya elimu ya hedhi itolewe kwa makundi yote, kwa kuwa baadhi ya wanafunzi wa kiume huwadhihaki wasichana pale wanapoingia katika hali hiyo.

Anataja kingine, ni kwa baadhi ya wazazi wa kiume wanaposhindwa kuwahudumia watoto wa kike na kuona hilo ni jukumu la mwanamke na sio la baba.

"Wapo mabinti wanaishi na mzazi mmoja wa kiume, wanapokuwa katika hedhi ukiomba pesa unaambiwa hilo ni j ukumu la mwanamke na sio la mwanamume," anasimulia.

Binti huyo pia anawageukia kinamama, baadhi kila siku hucheza vikoba wanakotoa michango, lakini ni wagumu kugharmia bajeti za taulo za kike kwa mabinti zao.

# Tembo, simba wafungwa mikanda ya mawasiliano

**Na Romana Mallya**

WIZARA ya Maliasili na Utalii katika kukabiliana na migogoro baina ya binadamu na wanyamapori wakali na waharibifu, imeandaa na kuzindua Mkakati wa Kitaifa wa Utatuzi wa Migogoro baina ya Wanyamapori na Binadamu (2020 -2024).

Vilevile, imesema mkakati wa kitaifa wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara umefanyiwa mapitio na mkakati mpya wa miaka 10 (2020/2021-2030/2031) unaandaliwa.

Waziri wake, Dk. Damas Ndumbaro, aliyasema hayo jana bungeni alipowasilisha makadirio na mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Katika kutatua migogoro baina ya wanyamapori na binadamu, Dk. Ndumbaro alisema mkakati wao unalenga kuweka njia bora na endelevu za kukabiliana na wanyamapori na kuimarisha uhusiano na wananchi kwa kuhakikisha jamii inayoishi karibu na maeneo ya hifadhi inapata elimu ya namna ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu.

"Wizara imeendelea kutoa elimu ya kukabiliana na wanyamapori wakali na waharibifu kwa jamii zinazoishi karibu na maeneo ya hifadhi," alisema.

Dk. Ndumbaro alisema wizara imeendelea kutumia teknolojia ya kufuatilia nyendo za tembo, simba na fisi kwa kuwafunga vifaa maalum (radio collars) ili kurahisisha ufuatiliaji wa wanyamapori hao.

Alisema katika kufanikisha hilo, jumla ya makundi 42 ya tembo katika Mfumo Ikolojia Serengeti, Ziwa Natron na Manyara -Tarangire; na makundi 17 ya simba katika Mifumo Ikolojia Serengeti na Ruaha -Rungwa wamevishwa mikanda ya mawasiliano ili kuwezesha ufuatiliaji wa mienendo yao.

Alisema wizara kwa kushirikiana na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu imeendelea kufanya doria na kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna ya kukabiliana na tatizo la fisi wanaokula mifugo ikiwa ni pamoja na kuharibu maficho ya wanyamapori hao.

"Hatua nyingine zilizochukuliwa na wizara ni pamoja na kuendelea kutoa kifuta jasho na kifuta machozi kwa wananchi walioathiriwa na wanyamapori wakali na waharibifu ambapo jumla ya Sh. bilioni 1.252 zimelipwa.

Pia alisema wizara kwa kushirikiana na wadau imefanya tathmini ya shoroba kwa ajili ya kuandaa mikakati ya kuzihifadhi ili kuruhusu mtawanyiko wa wanyamapori na matokeo yameonyesha uwapo wa shoroba 61.

Kati ya hizo, shoroba 20 zimeonekana kuhitaji kupewa kipaumbele ili kuzirejesha katika hali yake ya awali zisiendelee kuvamiwa.

Waziri huyo alisema katika kuimarisha ulinzi, usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori, wamekamilisha maandalizi ya Kanuni na Amri za Jumla za Jeshi la Uhifadhi la Wanyamapori na Misitu; na kuandaa Mtaala wa Jeshi la Uhifadhi wa Wanyamapori na Misitu utakaotumika kutoa mafunzo kwa watumishi.

Pia, alisema wamepunguza bei ya usajili wa eneo la kuuzia nyamapori kutoka Sh. 250,000 hadi Sh.100,000 ili kuwawezesha wananchi wengi kuzifungua na kunufaika na rasilimali za wanyamapori.

Alisema mkakati wa kitaifa wa kupambana na ujangili na biashara haramu ya nyara umefanyiwa mapitio na mkakati mpya wa miaka 10 (2020/2021 -2030/2031) unaandaliwa.

Waziri Ndumbaro alisema katika kutatua migogoro ya ardhi baina ya wananchi na maeneo yaliyohifadhiwa, wizara kwa kushirikiana na wadau imehakiki mipaka ya hifadhi yenye urefu wa kilometa 97, kusafisha kilometa 1,554 na kuweka alama za mipaka 788 na mabango 180 katika maeneo ya hifadhi za misitu na wanyamapori.

Alisema jumla ya miti 6,250 imepandwa katika mipaka ya hifadhi 84 ya misitu ya asili.

"Wizara imeweka jumla ya maboya 66 katika Hifadhi za Taifa Saadani na Rubondo kama alama za mipaka kwenye eneo la maji.

"Wizara imeanza mchakato wa kuhakiki mipaka kwenye maeneo ya malikale na urithi wa utamaduni ikiwamo vituo vya Kalenga, Amboni, Engaruka, Engaresero, Isimila, Tembe la Kwihara, Ujiji Kigoma, Tongoni, Kunduchi na Kaole," alibainisha.

Alisema katika kuliendeleza Jiji la Dodoma kuwa la kijani, kwa kushirikiana na wadau hadi Aprili, mwaka huu wamepanda jumla ya miche 3,505,280.



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akizungumza na viongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwenye ukumbi wa Ofisi ndogo ya Waziri Mkuu,Magogoni jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakamatwa tuhuma kuwavamia masista

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linawashikilia watu tisa kati ya 12 wanaotuhumiwa kuvunja nyumba wanayoishi masista wa Kanisa Katoliki kisha kuwaibia na kuwajeruhi kwa kutumia bisibisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, alisema jana kuwa tukio hilo lilitokea Mei 31 majira ya saa saba usiku huko Ngoiga Vikuge, Kata ya Kongowe, Wilaya ya Kibaha.

Alidai kuwa watu hao walivunja milango ya nyumba wanayoishi masista hao na kuingia ndani.

Kamanda huyo alisema watu hao waliokuwa 12 walivunja milango ya nyumba hizo kwa kutumia marungu na bisibisi na kuiba kompyuta mpakato mbili, simu mbili, vitu mbalimbali na fedha taslim Sh. milion 2.5 na kutokomea kusikojulikana.

Kamanda Wankyo alisema katika tukio hilo, masista wawili walijeruhiwa huku mmoja akichomwa na bisibisi usoni.

Alisema katika msako wa awali, watu tisa walikamatwa na wanashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano huku msako ukiendelea kwa waliobaki.

Alisema masista hao wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Tumbi kutokana na majeraha waliyopata.

# Wachimbaji waonywa imani za kishirikina

**Na Marco Maduhu,** KAHAMA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wameonywa kuendekeza imani za kishirikina kwenye migodi wakati wa utafutaji mali, kuepuka vifo vya watu wasio na hatia.

Mwenyekiti wa Shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu wilayani Kahama (SHIVYAWATA), Michael Mkanjiwa, alisema hayo juzi ofisini kwake alipotembelewa na gazeti la Nipashe.

Alisema asilimia kubwa ya wachimbaji wadogo wa madini, huendekeza imani za kishirikina na kwenda wa waganga wa kienyeji kupigiwa ramli chonganishi, na kusababisha mauaji ya watu wasiokuwa na hatia wakiwamo wenye ualbino wakiamini watapata madini.

"Naomba wachimbaji wadogo wa madini, waachane na imani hizi potofu za kishirikina wakati wa utafutaji madini, bali washirikishe wataalamu kuwapimia eneo hilo kama lina dhahabu, na siyo kutoa uhai watu wasiokuwa na hatia wakiamini watapata madini. huko ni kujidanganya tu," alisema Mkanjiwa.

"Sisi kama shirikisho la vyama vya watu wenye ulemavu wilayani Kahama, tunapiga sana vita masuala ya kuendeleza imani za kishirikina, kwa kuamini watu wenye ulemavu viungo vyao vina bahati ya kupata mali, imani hiyo siyo kweli ni kuibiwa pesa tu na waganga hawa wa kienyeji," aliongeza.

Katika hatua nyingine Mkanjiwa aliiomba derikali, kufanya msako wa kubaini waganga wa kienyeji ambao bado wanaendekeza masuala ya upigaji ramli chonganishi, ili kuwachukulia hatua kali za kisheria na kuzuia mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

Kwa upande wake Mkaguzi msaidizi wa Jeshi la Polisi wilayani Kahama, Eliasi Sikanda, akimwakilisha Mkuu wa Polisi wilayani humo, ambaye pia ana husika na polisi jamii, alisema wameanza kutoa elimu kwa jamii wakiwamo wachimbaji madini kupitia mikutano ya hadhara kuacha masuala ya kuendekeza imani za kishirikina.

Alisema mpaka sasa wameshafanya mikutano mitatu, na kubainisha pia watafanya misako ya kubaini waganga wa kienyeji ambao wanapiga ramli chonganishi, huku akiwaonya vijana kuacha tabia ya kukodiwa kwenda kukata mapanga watu wasiokuwa na hatia, bali wafanye shughuli zingine halali za kuwaingizia kipato.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MUSA M. KADINDA** anatangaza kupotelewa kadi yake ya gari Toyota corolla mali ya m/s. lasting last ltd yenye usajili Namba **T 177BNA** yenye **CHASSIS NO NZE1203028382.** Kwa yoyote atakaye ona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **RB Na. MOR/MOR/RB/ 272410/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **MUSA M KADINDA** anatangaza kupotelewa kadi yake ya gari Toyota Carina mali ya m/s. lasting last ltd yenye usajili Namba **T 608BPB** yenye **CHASSIS NO AT2116056134.** Kwa yoyote atakaye ona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **RB Na. MOR/MOR/RB/ 272425/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.170/2021**

Ombi la **SARAH MAURUSI NGOMBALE** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **TOPERA SAID KASHINDE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe **09/07/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 04/06/2021**

HAKIMU

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**LA WILAYA YA LINDI**
**LILILOPO LINDI**
**MAOMBI NAMBA 9 YA MWAKA 2021**
**OLIVER JIVAVA**
**SANGA.............................MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**MANASE AMBONILE**
**MWAKIKISI..................MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**

**MANASE AMBONILE MWAKIKISI** popote ulipo **FAHAMU** kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe **24 June 2021** saa **02:30 asubuhi.**

**UNAAMBIWA** kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la zamani la Halmashauri ya Wilaya ya Lindi lililopo Manispaa ya Lindi siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria. Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Bazara.

**FAHAMU KWAMBA** kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kuamuriwa dhidi yako.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe **03 June, 2021.**

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**
**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**MIRATHI NA 47 YA MWAKA 2021**
**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**
**CECILIA ADAM KIONDO**
**MWOMBAJI/WAOMBAJI**
**ANCAS CARLOS KIONDO**
**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa mirathi kwa waombaji/mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya tarehe 17th mwezi wa **JUNE 2021**

Imewasilishwa Dar Es Salaam leo tarehe **11th mwezi MAY 2021.**

NAIBU MSAJILI

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA**
**WILAYA YA ILEMELA**
**SHAURI LA MADAI YA PESA NAMBARI 189 YA 2020**
**MADAI...................................HUSSEIN MAHAMUD**
**DHIDI YA**
**MDAIWA.........................................KIJAKAZI REHANI**
**KWA KIJAKAZI REHENI.**

**YAH- KUITWA SHAURINI**

**POPOTE PALE ULIPO**

Fuhamu kwamba mdai ameleta madai yake mahakamani dhidi yako. Madai haya yamepangwa kusikilizwa tarehe **07/06/2021.**

Fahamu kwamba unatakiwa kuhudhuria mahakamani wewe mwenyewe siku hiyo bila kukosa. Kutohudhuria kwako kutaifanya mahakama hii iendelee na shauri hili bila wewe kuwepo na kulitolea uamuzi.

Imetolewa kwa amri na mhuri wa mahakama hii leo tarehe **04/06/2021.**

.........................................
**C.H.KAAYA**
**KAIMU HAKIMU MFAWIDHI.**
**MAHAKAMA YA MWANZO ILEMELA**
**MWANZA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Baruapepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaawa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 04-06-2021**

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya JUMATATU tarehe 07-06-2021 kampuni za ALFRED AROBOGAST TARIMO na OTTO MARK INVESTMENT LIMITED zitasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka DAR ES SALAAM kuelekea ARUSHA kupitia DODOMA. Gari hizo zenye namba za usajili zenye vipimo vyake:

   **T 269 DPX / T 270 DPX**
   **T 143 CFT / T 555 DRM**

   **T 548 CKZ / T 386 CHR**
   **T 194 BZX / T 957 BQT**

**Zote zina VIPIMO: UREFU 22 UPANA 4.6 KIMO 5.4**

2. Gari hizo zinatoka DAR ES SALAAM kuelekea ARUSHA kupitia DODOMA. Gari zitasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni).

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

## TUNAPANGISHA

PR STADIUM HOTEL ILIYOPO KARIBU NA UWANJA WA TAIFA TEMEKE TUNAPANGISHA “BAR” NA “LOUNGE” KWA BEI NAFUU SANA. KWA MAWASILIANO PIGA SIMU NO: 0764 822 509 / 0762 215 470.

**Uza,**
**Chenye Thamani**
**Kubwa Kwa Kutangaza**
**Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**Kwa Habari Motomoto**
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam.**
**Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HADITHI

MWANZONI ilionekana ni fahari. Wazazi kupata mtoto wa kike. Akaja kuwa msichana mzuri aliyeumbwa akaumbika na kutamaniwa na kila mtu ni sifa kubwa. Wakati mwingine mzazi hupata hata vizawadi vidogo kutoka kwa watu mbalimbali bila kujua kuwa nia ni kutengeneza mazingira kwa binti yao. Kinyume chake mzee Ngoma na mkewe Fatuma wanapata mtoto wa kike Bishada ambaye anaondokea kuwa tishio kwenye kijiji cha Mtakuja kwa urembo wake. Badala ya kuwa tija na faraha kwa wazazi wake anageuka kuwa balaa. Wazazi wanakuwa hawana amani kutokana na vitisho mbalimbali ikiwemo kuuawa kutoka kwa watu mbalimbali ndani na nje ya kijiji hicho.

# Aolewe au afe-9

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

Natanguliza kwanza samahani kwa sababu sitaki kukukumbusha kilichotokea jana. Lakini naomba tu uniambie kwa nini yule jamaa aliamua kufanya hivyo? Na kuna nini kwenye kijiji hiki, maana kuna maneno niliyasikia wakati namkabidhi pale kwa Mwenyekiti wa Kijiji yalikuwa yanaongelewa."

Bila ya samahani. Bila ya kuacha neno lolote. Bishada alimhadithia Denis kila kitu kilichotendeka kwenye kijiji hicho hadi kufikia pale alipomkuta.

"Kwa hiyo mna wiki moja tu ya kukaa hapa?" Ndiyo.

"Na wewe bado hujaamua kukubali barua yoyote ya uchumba?"

Bishada alisita kwanza. Kwa mara ya kwanza akamungalia mgeni yule kwa sekunde nyingi kuliko zote tangu afike pale akajibu "Ndiyo". Alipojibu akamuangalia tena.

"Kwa wewe sitokubali uondoke." Jibu hilo lilionekana kumfurahisha Bishada. Alitoa tabasamu pana.

"Kwa nini?" Aliuliza.

"Sijamzoea yoyote kwenye kijiji hiki zaidi yako. Ukiondoka nitabaki na nani?"

"Mbona wewe mwenyewe unakaa kwa muda tu kwa ajili ya mashamba ya mjomba wako, si utaondoka na wewe?"

"Nitaondoka na wewe. Au na mimi utanitosa?" Aliuliza kwa utani.

Bishada alitabasamu na uso akauelekeza kuangalia chini."

"Haya mama, twende nyumbani kwenu, sijui umenipikia nini."

Bishada aligeuza kichwa kwa mbwembwe. "Wali kuku." Aliongea kwa sauti ya chini ya kunong'oneza.

"Muongo."

"Kweli tena."

"Haya kwenu mimi sikujui. kwa hiyo nishike mkono."

Bishada aliangua kicheko kikali ambacho kilitoka bila hiyari yake. Akamshika mkono Denis.

"Haya twende." Wote wawili walijikuta wakiangua vicheko vya furaha.

**********************

Ilikuwa ni siku ya kukumbukwa. Si kwa Baba na Mama Bishada tu, bali kwa binti mwenyewe na Denis.

Chakula kililiwa huku wakiongea mengi. Denis aliwaelezea ujio wake kijiji pale ulikuwa ni wa kumalizia kupata hati za mashamba ya mjomba wake kwa sababu mrithi halali ni yeye.

Mzee Ngoma na mkewe Fatuma walikuwa wanamfahamu vema mzee Malilo ambaye ni mjomba wa Denis.




**Amezaliwa na dada wa mzee Malilo ambaye aliolewa, Dar es Salaam. Alibahatika kupata watoto watatu wawili wa kiume na mmoja wa kike. Mzee Malilo kwa kuona kuwa hakuwa na mtoto, aliandikisha mali zake kwa Denis. Ndiye aliyekuwa akimpenda zaidi kuliko mtoto yoyote wa dada yake.**

Alikuwa ni mtu safi, mkarimu na mcheshi. Ni mzee ambaye mkewe alianza kufariki kabla yake.

Kwa bahati mbaya hawakubahatika kupata mtoto. Mzee Malilo hakuoa mwanamke yoyote baada ya kufariki mkewe, hivyo aliishi peke yake kwa miaka mitano naye akafariki.

Ndiyo maana hakukuwa na mrithi yoyote zaidi ya Denis, au Denny kama anavyopenda kujiita mwenyewe.

Amezaliwa na dada wa mzee Malilo ambaye aliolewa, Dar es Salaam. Alibahatika kupata watoto watatu wawili wa kiume na mmoja wa kike.

Mzee Malilo kwa kuona kuwa hakuwa na mtoto, aliandikisha mali zake kwa Denis. Ndiye aliyekuwa akimpenda zaidi kuliko mtoto yoyote wa dada yake.

Ni kwa sababu Denis naye alionekana kumpenda mjomba wake na mara kwa mara wakati wa likizo alikuwa wakienda kumtembelea, wakitembezana shambani na sehemu zingine kiasi cha kumfariji sana mzee huyo.

Ndugu zake wengine hawakupenda sana mazingira ya kijijini, kwa hivyo hawakupenda kwenda kwa mjomba wao na hata kama wakienda hubaki nyumbani tu.

Ilipata saa 1:00 usiku, Denis alipoaga anataka kwenda nyumbani.

"Bishada msindikize mwenzako."

"Hapana mama, mwache tu akae. Umeshakuwa usiku na giza limeingia, itakuwa si vizuri sana, ila kesho mimi nitapitia kuwaona." Alijibu.

Denny na Bishada waliagana na kupena mikono. Denny aufinya kidogo. Bishada akatabasamu.

Tabasamu ambalo mzee Ngoma na mkewe waliliona pia. wakaangalia. Nao pia wakatabasamu bila kuonekana na hao waliopeana mikono.

Alitembea kiasi cha mita 500 hivi kuelekea nyumbani alikofikia kwa mjomba wake.

Ndipo alipogundua kuwa amesahau saa yake ambayo alikuwa ameiweka chini ya mkeka wakati akila.

Alisimama na kujiuliza kama arudi au aendelee. Kwa akili ya haraka haraka ilimtuma arejee. Kwa sababu kwanza hakuna yoyote kati ya Bishada na wazazi wake waliokuwa wanajua kuwa alivua saa na kuiweka kwenye mkeka, vinginevyo asingekuwa na wasiwasi kwani wangemuhifadhia.

Pili, si Bishada wala wazazi wake waliokuwa na simu za mkononi kuweza kuwapigia na kuwaambia waangalie pale alipoiweka ili aihifadhi.

Hivyo wazi zuri alililoliona ni kurudi alikotoka. Wakati akikaribia alianza kusikia sauti za watu ambao alikuwa na uhakika kuwa hazikuwepo hapo mwanzo.

Kwanza ni sauti za mzozo hivi, halafu za wanaume. Wakati anaondoka aliacha mwanaume mmoja tu ambaye ni mzee Ngoma.

"Toka nje wote. Kaa pale. Yuko wapi yule bwege wenu?" Denny alisikia sauti ya mtu mmoja ikiuliza kwa ukali.

Hakukuwa na jibu.

"Yoyote atakayepaza sauti ya kupiga kelele, panga litaishia shingoni mwake. Yuko wapi yule bwege wenu aliyekuja kijijini hapa na kutufanya wanaume wote hapa wajinga?"

"Ameshaondoka, amekwenda kwake." Lilikuwa ni jibu la mzee Ngoma.

"Sikiliza wewe mzee. Sisi tumekuja hapa kwa lengo moja. Kumuua binti yako Bishada na jamaa yake yule. Sasa kama hayupo, tunaanza na binti yake, halafu tunakwenda kumalizana na yule mgeni." Sauti nyingine ilisikika.

"Hapana hapana, msimuua binti yangu. Niueni mimi basi, huku muacheni hana kosa lolote..." Mzee ngoma alipaza sauti yenye hofu.

"Mzee hii tenda tu tumepewa sisi na watu ambao binti yako amewakataa, kwa hiyo hatuwezi kufanya kinyume na hapo."

Haraka Denny alijitosa kwenye kichaka ili kuangalia zaidi tukio hilo bila kuonekana.

Alichoona ni vijana wanne, mmoja akiwa ameshika panga, wawili fimbo na mmoja kisu.

Denny tayari alishaambiwa kila kitu kuhusu familia ile. Ni familia ambayo haipendwi kijijini hapo kutokana na msichana mrembo Bishada kukataa kuolewa na mtu yoyote hapo, hivyo amezua chuki.

Kwa maana hivyo alijua hakukuwa na msaada wowote utakaotolewa. Pia vijana wale kwa walivyojieleza ni kwamba wametumwa.

Alivuta taswira kama asingerudi sijui ingekuwaje. Alinyata na kusogea karibu. Alikuwa ameshawazungukia kwa nyuma. Sehemu ambayo wao wanaangalia mbele, yeye alikuwa nyuma yao.

Alijipapasa mfukoni, bastola yake ilikuwepo. "Ngoja niwafanyie mchezo mmoja ambao utakuwa mfano kwa kijiji kizima." Alijisemea.

Alichomoa bastola yake na kutoka kwenye kichaka haraka akielekea kwenye tukio.

"Nyie wapuuzi wekeni chini silaha zenu, vinginevyo nitamtoa mtu utumbo, pumbavu nyinyi." Alionguruma.

Uliofuatia hapo ni mshtuko. Kwa wahalifu ulikuwa ni mshtuko maradufu kwa sababu hawakutegemea kukutana na hali ile.

**INAENDELEA**

# BENTEKE AJIFUNGA PALACE HADI 2023



**LONDON,** England


CHRISTIAN Benteke amefanikiwa kuongeza mkataba wa kusalia Crystal Palace kwa miaka miwili zaidi na sasa atakaa hapo hadi ifikapo mwaka 2023.

Benteke alijiunga na Palace akitokea Liverpool miaka mitano iliyopita na akiwa Palace msimu huu amefunga mabao 10, na kufikisha 82 katika michezo 255 ya Ligi Kuu England aliyocheza.

Palace bado haijajua nani atakuwa mrithi wa aliyekuwa kocha wao, Roy Hodgson ila mweyekiti wa klabu hiyo ameamua kumwongeza mkataba mchezaji huyo kwa kuwa amekuwa sehemu ya muhimu sana ya mafanikio yao.

"Cristian amekuwa sehemu muhimu sana ya kusaidia Crystal Palace kwa miaka mitano iliyopita na tutaendelea kufanya naye kazi," alieleza Mwenyekiti, Steve Parish.

Benteke atawakilisha Ubelgiji katika michuano ya Euro 2020 majira haya ya joto na anatarajiwa kuonyesha mambo makubwa na kutoa mchango mkubwa akishirikiana na wakali kama, Eden Hazard, Kevin De Bruyne na Romelu Lukaku.



# Gallas: Arteta hakupaswa kufundisha Arsenal

**LONDON,** England

NYOTA wa zamani wa Arsenal, William Gallas amesema Mikel Arteta hakujiandaa kuwa kocha wa kikosi hicho cha washikabunduki.

Raia huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 43 anaamini Arteta hakufaa kuinoa timu hiyo.

Arsenal ilimpa kazi raia huyo wa Hispania baada ya kumfungashia virago, Unai Emery.

Mafanikio ambayo ameyapata Arteta ndani ya Arsenal ni kutwaa taji la FA msimu wa 2019/20 na Ngao ya Jamii.

Msimu wake kamili wa 2020/21 imeshuhudiwa Arsenal ikimaliza nafasi ya nane kwenye msimamo na itakosa michuano ya Ulaya kwa mara ya kwanza baada ya miaka 25.

Nyota huyo alicheza ndani ya kikosi hicho kuanzia 2006-2010 anaamini kwamba Arteta hakuwa tayari kupewa kazi hiyo kubwa katika kuitumikia Arsenal.

"Mikel Arteta bado hakuwa tayari kuiongoza timu kama Arsenal," alisema Gallas akiambia Sky Sport.

"Sawa alikuwa kocha msaidizi Manchester City, lakini hakuwahi kuongoza timu hiyo ni tofauti kabisa."

# Madrid wampa mkataba Vazquez

**MADRID,** Hispania

LUCAS Vazquez amesaini mkataba wa miaka mitatu na Real Madrid na raia huyo wa Hispania amesema atakuwa na nafasi ya kuongeza historia ndani ya klabu hiyo.

Baada ya kumwaga wino kwenye mkataba mpya alijadili mafanikio na kila kitu anachotarajia kukipata ndani miaka ijayo akiwa na Los Blancos hao.


"Hii inamaana kubwa kwangu na ninajivunia, ni maalumu," alisema baada ya kusaini makataba mpya na Real Madrid.

"Ndoto yangu inaendelea hapa, ambayo ni nyumba yangu, na kitu ambacho nahisi ni sehemu yangu sana.

"Nimefurahi sana kuongeza mkataba wangu na kufurahia kuwa mchezaji wa Real Madrid hadi 2024. "Mimi ni mchezaji wa klabu ambaye nimekua na maadili ya Real Madrid na hii inafanya familia yangu na mimi kufurahi sana.

"Real Madrid wana maadili yaliyowekwa vizuri, kufanya kazi kwa bidii, kuheshimu wengine, unyenyekevu... Haya mambo hayawezi kujadiliwa maishani na kwenye mpira.

"Nimecheza mara 240 lakini nitapambana kuhakikisha kuwa kuna mengi zaidi yajayo."



# Arsenal yamwania Sterling

**LONDON,** England

ARSENAL iko mstari wa mbele katika mbio za kunasa saini ya Raheem Sterling katika dirisha hili la uhamisho wa majira ya kiangazi huko Ulaya.

Sterling ametajwa kuwa mmoja wa wachezaji ambao Manchester City inaweza kuwafungulia mlango wa kutokea ili kupata pesa za kufanikisha usajili wa straika wa Tottenham, Harry Kane.

Winga huyo Mwingereza, amepoteza nafasi kwenye kikosi cha kwanza cha Kocha, Pep Guardiola tangu alipoibuka kinda, Phil Foden.

Baada ya kuondoka, Sergio Aguero, Manchester City akili yake imewekeza kupata mrithi wake na inapiga hesabu za kunasa saini ya Kane ambaye thamani yake inatajwa kuwa pauni milioni 150.

Kupata pesa ndefu hivyo, City itahitaji kuuza mastaa wake na Arsenal inatazama hilo kama fursa ya kumnasa Sterling, ambaye ilikuwa ikimsaka kwa muda mrefu.

Arsenal ilimkosa Sterling mwaka 2010 alipokuwa QPR na kuzidiwa ujanja na Liverpool iliyomnyakua kwa pauni 600,000.

Lakini, kwa sasa Kocha, Mikel Arteta ana nafasi ya kumsajili mkali huyo kama atakuwa siriazi. Na kitu kizuri ni kwamba Arsenal ipo tayari hata kumlipa mshahara wa Sterling, anayelipwa Pauni 300,000 kwa wiki.




# MAGUIRE KUIKOSA CROATIA EURO 2020




**LONDON,** England

IMETHIBITISHWA kuwa beki, Harry Maguire atakosa mchezo wa awali wa michuano ya Euro baada ya kuwa majeruhi hiyo, kwa mujibu wa Kocha wa Timu ya Taifa ya England, Garreth Southgate.

"Timu ya madaktari imekuwa naye Manchester kwa matibabu, hawezi kusafiri nasi kwa sababu bado hajawa fiti vya kutosha hivyo atakuja akitokea Poland, huo ndio ugumu," alisema Southgate.

"Mchezo wa kwanza utakuwa mgumu sana, hakuna haja ya kuelezea sana katika hilo" ameongeza Southgate.

England inakutana na Croatia katika mchezo wa kwanza utakaochezwa Juni 13, mwaka huu kwenye Uwanja wa Wembley.

Beki huyo aliumia katika mchezo wa Ligi Kuu England dhidi ya Aston Villa uliochezwa Mei 9, mwaka huu.

# *Ancelotti afunguka hatima ya Ramos*

**MADRID,** Hispania

CARLO Ancelotti amesema hana mashaka yoyote kuhusu kurejea Real Madrid, lakini pia hana pingamizi la kuondoka kwa nahodha, Sergio Ramos.

Ancelotti, ambaye aliwahi kuifundisha klabu hiyo kuanzia mwaka 2013 mpaka 2015 aliwasili kwenye uwanja wa mazoezi wa Real Madrid juzi.

Mtaliano huyo mwenye umri wa miaka 61 amesaini mkataba wa miaka mitatu kuchukua nafasi ya msaidizi wake wa zamani, Zinedine Zidane aliyejiuzulu wiki iliyopita.

Ancelotti alisema hajapata muda wa kujadili usajili au benchi lake la ufundi na Rais, Florentino Perez na kukitetea kikosi cha sasa akiwamo Gareth Bale na Eden Hazard kumaliza msimu bila taji.

"Nilimwona rais mapema, tulizungumza kiasi, ilikuwa kwa haraka tu," alisema Ancelotti. "Hatukupata muda wa kuzungumza, tutaanza kazi siku chache zijazo, namshukuru rais kuwa hapa ni muhimu sana kwangu."

Aliongeza: "Nadhani kikosi kiko vizuri, kuna mchanganyiko wa wachezaji wenye uzoefu akiwamo [Toni] Kroos, [Luka Modric, Ramos, Bale, [Karim] Benzema na wachezaji chipukizi wenye viwango: Vinicius Junior, Rodrygo, [Federico] Valverde kikosi ni kikubwa, tunatakiwa kupunguza kidogo."


"Nadhani kwa kikosi hiki tunaweza kushindana," aliongeza Ancelotti.

"Kwa kikosi hiki na bila kuwa na wachezaji wa mkopo kama Bale, [Martin] Odegaard, [Dani] Ceballos, Madrid inakwenda kwenye nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa na kupambana kwa La Liga."

Ancelotti alisema anahitaji kufanya mambo kwa haraka na kuzungumza kuhusu mkataba wa Ramos kabla ya mambo mengine.

"Ndio kwanza nimefika, natakiwa kuzungumza na klabu kuhusu yote hayo... nawafahamu wachezaji wote ni vizuri nimerejea na kufanya nao kazi na Sergio Ramos akiwa mmoja wao."

"Amekuwa mmoja wa wachezaji walioleta mafanikio kwenye klabu hii, anazungumzia kuhusu kuongeza mkataba lakini ni kama nilivyosema jana (juzi) nilikuwa Liverpool, nitakapofahamu mambo yote nitazungumza wazi zaidi."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: BADO SIJAFIKIA UBORA WA MESSI, RONALDO

●●● Mfaransa huyo amekataa kulinganishwa na mastaa hao na kusema kufanya hivyo si heshima...

**PARIS,** Ufaransa

NYOTA wa kikosi cha PSG, Kylian Mbappe amesema kulinganishwa na nyota wa soka duniani, Lionel Messi na Cristiano Ronaldo ni kutowatendea haki wachezaji hao.

**Mbappe amesema wachezaji hao wawili hawalinganishiki kwa kuwa wamevunja sheria zote za takwimu.**

Nyota huyo ameweka wazi kuwa ikiwa itakuwa namna hiyo basi atakuwa anawakosea heshima wachezaji hao ambao ni mastaa katika ulimwengu wa soka.

Mbappe na nyota wa Borrusia Dortmund, Erling Haaland wanatajwa watatawala ulimwengu wa soka wakati ujao kwa miaka mingi na kuchukua utawala wa nyota hao wawili ambao muda wao kwa sasa unazaidi kuwaacha taratibu.

Umri wake ni miaka 22 tayari ameshatwaa Kombe la Dunia, mataji manne ya Ligi Kuu Ufaransa, (Ligue 1), Kombe la FA Ufaransa mara tatu na Kombe la Ligi mara mbili pamoja na kushika nafasi ya pili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2020.

Mbappe amesema:"Kama utajiambia mwenyewe kwamba utafanya vizuri zaidi ya hao itakuwa ni kiburi kilichopitiliza.

"Ni kukosa heshima kujilinganisha na wachezaji kama Messi na Ronaldo, hao ni wachezaji ambao wamefanya kila kitu kwenye soka.

"Ni sawa na kusema wamevunja sheria zote za takwimu, hivyo hawapaswi kulinganishwa na mchezaji yoyote kwa sasa.

"Binafsi naona ni kiburi kikubwa mimi kulinganishwa na wachezaji hawa."

## ZISIKUPITE

### ZAHA KUONDOKA PALACE

MSHAMBULIAJI wa Ivory Coast, Wilfried Zaha mwenye umri wa miaka 28, ameieleza Crystal Palace kwamba anataka kuondoka kabla ya msimu wa mazoezi kuanza. ***(Times)***

### SANTO ANUKIA EVERTON

EVERTON iko tayari kutoa ofa ya mkataba wa miaka mitatu kwa aliyekuwa Kocha Mkuu wa Wolves, Nuno Espirito Santo mwenye umri wa miaka 47. ***(Nicolo Schira via Star)***

### ARSENAL, VILLA VITANI

ARSENAL na Aston Villa wametenga rasmi vitita vya fedha kwa ajili ya kumwania winga wa Argentina anayechezea Norwich anayesemekana kwamba thamani yake ni pauni milioni 40, Emi Buendia (24). ***(Sun)***

### BARCA KUMUUZA MORIBA

BARCELONA inasemekana iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Hispania, Ilaix Moriba mwenye umri wa miaka 18, licha ya timu za Manchester United, Manchester City na Chelsea kuonyesha nia ya kumtaka. ***(Mail)***

### RAPHINHA AGOMBEWA

LIVERPOOL inaongoza katika mbio za kuwania kumsajili winga, Raphinha kutoka Leeds, lakini Manchester United na Manchester City pia nazo zinamsaka mchezaji huyo raia wa Brazil mwenye umri wa miaka 24. ***(Gianluigi Longari via Express)***

### GUENDOUZI RASMI SOKONI

ARSENAL iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Ufaransa, Matteo Guendouzi, 22, kwa euro milioni 10. ***(Le10Sport via Calciomercato)***

### SULEMANA ATUA AJAX

KLABU ya Ajax imeipiku Manchester United katika kumsajili winga wa Ghana, Kamaldeen Sulemana mwenye umri wa miaka 19, kutoka FC Nordsjaelland. ***(Football Insider)***

### NIGUEZ MAMBO SAFI

ATLETICO Madrid iko tayari kutoa ofa kwa kiungo wa kati wa Hispania, Saul Niguez mwenye umri wa miaka 26, ambaye awali aliwahi kuhusishwa na mpango wa kujiunga na Manchester United. ***(Marca)***

### BAKAYOKO ANUKIA ITALIA

KLABU ya Fiorentina ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Ufaransa, Tiemoue Bakayoko mwenye umri wa miaka 26, kwa mkopo kutoka Chelsea msimu huu. ***(Fabrizio Romano, Twitter)***

### ALLEGRI KUMBAKIZA RONALDO

KOCHA anayerejea Juventus, Massimiliano Allegri alikutana na wafanyakazi wa Juventus Alhamisi, huku hatima ya mshambuliaji Mreno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, ikiwa kipaumbele katika orodha ya ajenda zake. ***(Goal)***

HABARI MICHEZO

# ILANFYA ATANGAZA 'UBABE' AKIJIPANGA KURUDI SIMBA SC

Na Shufaa Lyimo

MSHAMBULIAJI wa Simba, Charles Ilanfya ambaye kwa sasa anaichezea KMC kwa mkopo amesema anajiandaa kurejea akiwa katika kiwango bora kwa mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye msimu ujao wa ligi hiyo.

**Simba ilimsajili Ilanfya kutoka kwa KMC, lakini ikaamua kumrejesha katika timu yake ya zamani baada ya kukosa namba kwenye kikosi hicho cha Wekundu wa Msimbazi.**

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ilanfya alisema baada ya kumaliza mkataba wake wa mkopo ndani ya KMC, amejiandaa kurejea akiwa na makali zaidi huku pia akiahidi kuonyesha ushindani kwa nyota wenzake walioko Simba. Ilanfya alisema atacheza kwa juhudi na atapambana ili kutimiza malengo yake ya kuitumikia Simba kwa mafanikio kama ilivyotarajia wakati inamsajili.

"Kwa sasa mkataba wangu na KMC bado haujamalizika, ukimalizika nitarudi Simba kwenda kupambana, nimejiandaa kwenda kutekeleza vyema majukumu yangu kama ilivyokuwa awali kabla sijaletwa hapa kwa mkopo," alisema Ilanfya.

Mshambuliaji huyo alisema anawaomba mashabiki na wanachama wa Simba kumpa ushirikiano kwa sababu amejiandaa kutoa mchango mkubwa katika kikosi hicho kwenye msimu ujao ambao pia unatarajiwa kuwa na ushindani zaidi.

"Ninawaomba wadau wanipokee vizuri, wanipe ushirikiano ili nitimize mikakati yangu nilijiwekea, naahidi nitajituma licha ya ukweli ndani ya kikosi cha Simba kuna ushindani mkubwa wa kupata namba," alisema mshambuliaji huyo.

Kuhusu mchezo wa KMC dhidi ya Dodoma Jiji FC utakaochezwa Julai 17, mwaka huu alisema kikosi chao kinaendelea vizuri na maandalizi na wachezaji wamejipanga kumaliza msimu kwa kusaka matokeo chanya.

"Tunataka kuendeleza heshima yetu msimu huu, tutaivaa Dodoma Jiji kwa umakini na utulivu, wao pia watakuwa wamejipanga kusaka ushindi, tunatarajia ushindani kwenye mchezo huo na mechi nyingine zilizobakia," alisema nyota huyo.



Msanii mkongwe wa taarabu nchini, Khadija Kopa (kushoto), ambaye ni balozi wa DStv Tanzania, akizungumza katika uzinduzi wa kampeni mpya ya Michuano ya Ulaya iliyopewa jina la 'Biriani la Ulaya' itakayoonyeshwa na DSTV kwa lugha ya Kiswahili kupitia chaneli ya Supersport EURO. Kulia pia ni balozi wa kampuni hiyo, Rommeo George. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Shule tatu kushiriki tamasha la Azam FC leo

Na Saada Akida

KATIKA kuhakikisha wanakuwa karibu na jamii, uongozi wa Azam FC ambayo inashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara umeandaa tamasha la michezo litakalofanyika leo kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Meneja wa Mauzo na Masoko wa Azam FC, Tunga Ally alisema tamasha hilo litashirikisha wanafunzi wa Shule za Msingi ambao watachuana katika mchezo wa mpira wa miguu na wavu.

Tunga alisema lengo la kuandaa tamasha hilo ni kukuza na kuwa nafasi wanafunzi wenye vipaji kuonekana huku vile vile wakikuza nembo ya klabu yao.

Kiongozi huyo alisema tayari shule tatu za Msingi zimeshathibitisha kushiriki kwao huku wakitangulia kufanya ziara kwenye uwanja huo unaotumika pia michezo ya kimataifa ili kuangalia uwekezaji uliofanyika.

"Licha ya kutaka kuendeleza michezo mashuleni lakini pia kwetu ni nafasi nzuri ya kutengeneza na kupata mashabiki wapya wa baadaye, ndani ya miaka mitano ya kuuza nembo ya klabu itokanayo na vitu mbalimbali kama jezi," alisema Tunga.




Mkurugenzi wa Kampuni ya Umbro Afrika Kusini, Byron Mulholland (kulia), baada ya kusaini mkataba wa udhamini wa mashindano ya Kombe la Ndondo mwaka huu. Katikati ni Mkurugenzi wa Kamati ya Maandalizi ya michuano hiyo, Shaffih Dauda. **NA MPIGAPICHA WETU**

## *Umbro yajitosa kudhamini Ndondo Cup*

Na Mwandishi Wetu

KAMPUNI ya kutengeneza vifaa vya michezo UMBRO ya nchini Afrika Kusini imeingia makubaliano na Taasisi ya Michezo ya Shadaka kwa ajili ya kutengeneza vifaa vya michezo vitakavyotumika katika mashindano ya Kombe la Ndondo kwa mwaka huu, imeelezwa.

Kwenye makubaliano hayo, UMBRO imekubali kutengeneza jezi za timu 32 zitakazocheza kuanzia hatua ya makundi msimu huu pamoja na jezi kwa ajili ya waamuzi watakaochezesha michuano hiyo.

UMBRO pia itatoa mipira yenye ubora uliothibitishwa na Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA), ambayo ndio itatumika kwenye michuano ya msimu huu.

"Katika malengo yetu ya kuwa mashindano bora ya mtaani Afrika, Ndondo Cup mara zote inaangalia kwenye kutengeneza ushirikiano na mradi mkubwa, ndio maana tumeamua kushirikiana na UMBRO"-alisema Shaffih Dauda, Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya michuano ya Ndondo Cup.


Naye Mkurugenzi wa Umbro Afrika Kusini, Byron Mulholland alisema michuano ya Ndondo ni sehemu sahihi kwa vijana kuonyesha vipaji vyao vya soka Tanzania na mashindano hayo yanatoa mchango kwenye maendeleo ya mchezo huo ndani ya Afrika.

"Ushirikiano huu unaenda mbali zaidi ya Umbro kuingia kwenye soka la Tanzania, tunataka kufanya kazi na soka la ndani Afrika nzima. Tumefurahi kupata fursa hii na tunatarajia kuendelea kushirikiana zaidi na wengine ndani ya Tanzania," alisema Mulholland.

Michezo

Jumamosi Juni 5, 2021

Nipashe



Mbappe: Bado sijafikia ubora wa Messi, Ronaldo

UKURASA 22



Washambuliaji wa Simba, John Bocco (kushoto) na Chris Mugalu, wakifurahia bao la kwanza la timu hiyo katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ruvu Shooting iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza juzi. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

## AS Vita, Yanga SC bado ngoma mbichi

**Na Saada Akida**

WAKATI Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, akihitaji kufanya maboresho kwa kusajili nyota wenye uwezo wa juu kwa ajili ya msimu ujao, uongozi wa AS Vita ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), umeweka wazi hawajapokea ofa yoyote kutoka Yanga kuhusu kumhitaji beki wake wa kulia, Shabaan Djuma.

Hata hivyo mabosi wa klabu hiyo wameweka wazi wako tayari kupokea ofa kutoka kwa klabu yoyote ya Tanzania ikiwamo mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba na Azam FC.

Meneja wa AS Vita, Yves Diba, aliliambia Nipashe hawana taarifa rasmi za beki huyo kutakiwa na Yanga au klabu nyingine kama ambavyo inaelezwa na vyombo mbalimbali vya habari.

Diba alisema Djuma bado ni mchezaji wao halali kwa sababu ana mkataba wa miaka mitatu wa kuitumikia klabu hiyo, hivyo kama kuna timu nyingine inamhitaji italazimika kwenda kufanya mazungumzo na wao na wakifikia makubaliano watamuuza.

"Kama uongozi hatujui, tuna makubaliano na Yanga, lakini lazima Yanga waonyeshe utayari, nina imani na Injinia Hersi Said, ni rafiki yangu hivyo kama watakuwa tayari watafuata taratibu, bila shaka kuna Simba na Azam FC, milango iko wazi kwa yoyote anayehitaji huduma ya mchezaji huyo, ila kwa sasa hatutaweza kuzungumzia tetesi hizo," alisema kiongozi huyo.

Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haji Mfikirwa alisema wanaendelea kufanyia kazi mapendekezo yanayotolewa kuhusu nyota wapya watakaosajiliwa kwenye timu yao kwa sababu wanahitaji kuwa na kikosi imara kitakachoshindana katika michuano mbalimbali.

"Bado tunasubiri ripoti ya kocha ambayo itaeleza aina ya wachezaji anaowahitaji kwa ajili ya kuboresha kikosi chake, hizo tetesi za mara nyingi husemwa na watu, sisi kama viongozi hatutapelekeshwa na maneno yao, tutafanya usajili kwa kufuata utaratibu," alisema Mfikirwa.

Mbali na beki huyo Mkongomani, nyota wengine wanaotajwa kutua Jangwani ni pamoja na Dickson Abundo kutoka Dodoma Jiji FC, Ibrahim Ajib (Simba), Charles Manyama (Ruvu Shooting) na golikipa wa Tanzania Prisons, Jeremiah Kisubi ambaye atarithi mikoba ya Farouk Shikalo atakayeachwa.

# Simba yahitaji pointi 10 Bara

### Ni kwa ajili ya kulibakisha taji la ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania kwa...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya juzi kupata ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya Ruvu Shooting kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba sasa wanahitaji kuvuna pointi 10 ili kutangazwa mabingwa wapya kwa msimu huu wa 2020/21.

**Simba inayofundishwa na Mfaransa Didier Gomes na Msaidizi wake, Selemani Matola, imebakiwa na michezo saba ili kukamilisha msimu huu unaotarajiwa kumalizika ifikapo Julai 18, mwaka huu.**

Vinara hao ambao ni mabingwa mara tatu mfululizo juzi walifikisha pointi 67 baada ya kucheza mechi 27 na ili kufikia malengo waliyojiwekea, wanahitaji ushindi kwenye mechi tatu na sare moja ili kutawazwa tena wafalme wa ligi hiyo ambayo msimu ujao itashirikisha timu 16.

Iwapo Simba itafanikiwa kupata pointi hizo itafikisha jumla ya pointi 77 ambazo hazitafikiwa na timu nyingine yoyote ile kwa msimu huu.

Watani zao Yanga wako katika nafasi ya pili wakiwa na pointi 61 baada ya kushuka dimbani mara 29, wamesaliwa na mechi tano na endapo watashinda hizo zilizobakia, watafikisha jumla ya pointi 76. Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi ya juzi, Matola alisema baada ya ushindi huo sasa wana nafasi kubwa ya kuusogelea ubingwa kwa mara nyingine tena.

"Tunashukuru kwa ushindi huu. Wenzetu walikuja kwa kupania na kucheza mpira wa kutumia nguvu zaidi, lakini niwapongeze vijana wetu, walitulia na kufuata maelekezo tuliyowapa. Hawakutoka mchezoni kwa sababu tuliwaambia pointi tatu za leo ni muhimu zaidi, kwanza kwa ajili ya kutusogeza kwenye ubingwa, halafu ukumbuke Ruvu Shooting walitufunga mara ya kwanza," alisema Matola.

Nahodha huyo wa zamani wa Simba aliongeza uamuzi wa kuchezesha mastraika wawili katika mechi hiyo ulikuwa na lengo la kupata mabao ya mapema.

"Na kweli tukapata mabao, tukaituliza mechi, na baada ya kupata la pili uliona tulimtoa straika mmoja, Chris Mugalu na kumwingiza Mzamiru Yassin kwa sababu ya kusaidia kati pale kwa sababu Ruvu Shooting wana viungo wazuri," Matola alisema.

Naye Kocha Mkuu wa Ruvu Shooting, Boniface Mkwasa, alisema makosa yaliyoyafanywa na wachezaji wake na kuonyeshwa kadi nyekundu yaliwagharimu na kupelekea kupoteza mechi hiyo ya marudiano.

"Tulianza vizuri, lakini tulifanya makosa wenzetu wakatuadhibu. Kipindi cha pili tukapata kadi nyekundu ambayo ilitutoa kwenye mchezo na unapokuwa uko pungufu kwa timu kama ya Simba huwezi kuwamudu," alisema Mkwasa.

Simba itashuka tena dimbani Juni 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba kuwakabili wenyeji Polisi Tanzania halafu itaendelea na maandalizi kwa ajili ya mchezo wa hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Kombe la FA, dhidi ya Azam FC utakaochezwa kati ya Juni 24 na 27, mwaka huu Mjini Songea.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 9

9 770856 541002 >